# MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZILIZOPENDWA ZA KISWAHILI: MTAZAMO LINGANISHI WA DAUDI KABAKA NA KIKUNDI CHA MAROON COMMANDOS

**ONESMUS KIOKO MALELU**

**C50/CE/21211/2012**

**KAZI YA UTAFITI ILIYOWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**FEBRUARI, 2025**

# IKIRARI

Pendekezo hili la utafiti ni kazi yangu asili na halijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

**Mtahiniwa**

Sahihi: ____________ Tarehe: 28/2/2025

**Onesmus Kioko Malelu**

C50/CE/21211/2012

**Msimamizi**

Pendekezo hili la utafiti limewasilishwa kwa idhini yangu kama msimamizi katika chuo kikuu.

Sahihi: ____________ Tarehe: 18/3/2025

**Prof. Geoffrey K. King'ei**

Idara ya Kiswahili

Chuo kikuu cha Kenyatta

KISWAHILI AND AFRICAN LANGUAGES
10 MAR 2025
P. O. Box 43844-00100
NAIROBI
KENYATTA UNIVERSITY

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Benard Nthakyo na Froniser Benard kwa kunizaa, kunilea na kugharamia elimu yangu tangu utotoni. Kazi hii pia naitabaruku kwa mke wangu Caroline Mwikali ambaye alinitia moyo wakati wote nilipokuwa nikiishughulikia. Wanangu Olivia, Olesia na Bridgit. Siwezi nikawasahau kwa kunipa moyo wa kutia bidii. Mola awabariki.

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati kwanza zimwendee maulana kwa kunipa afya nzuri na akili razini kuikamilisha kazi hii.

Namshukuru pia msimamizi wangu kwa ushauri na maelekezo mazuri yaliyopatia utafiti huu msingi dhabiti. Asante sana Profesa King'ei kwa kuwa na moyo wa kunivumilia hadi tamati. Pia nashukuru mwenyekiti Profesa Githinji kwa kunishauri kwamba nisife moyo ipo siku ningemaliza. Bila nyinyi ningekata tamaa na kazi nisingemaliza.

Wanafunzi wenzangu Ibrahim Gathogo na Ingosi siwezi nikawasahau. Tulitembea pamoja katika kupanda hivi vidato vya elimu. Tulitiana moyo hadi tamati ya masomo yetu.

Mke wangu Caroline Mwikali na watoto wangu Olivia, Olesia na Bridgit, nawapongeza na kuwashukuru kwa kunishika mkono. Lile swali lenu "Daddy utamaliza lini?" lilinipa motisha ya kujishajiisha hadi nikamaliza mradi huu. Nawashukuru wazazi wangu kwa ushauri kwamba masomo hayana hatima. Mola awajalie baraka tele.

## MAELEZO YA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| Culture Week: | Juma ambalo Chuo Kikuu cha Kenyatta hutenga ili kuadhimisha tamaduni mbalimbali nchini |
| Nyimbo zilizopendwa: | Nyimbo za Kiswahili zilizotungwa miaka 50 iliyopita na ambazo zinatambulika na kutumiwa kama mfano bora katika jamii. |
| Santuri: | Chombo kinachotumiwa kutoa sauti za gramafoni. |
| Skiza Tunes: | Nyimbo au milio maalumu inayotumika kwenye simu kwa sasa kutumbuiza wateja wanaposubi kupokelewa. |
| You Tube: | Mtandao wa kijamii unaowawezesha watu kupitia video mbalimbali zikiwemo nyimbo. |
| Maudhui ibuka: | Mambo muhimu yanayochipuka kutokana na hali za maisha ya sasa. |
| Maudhui ya jumla: | Mambo muhimu ya kawaida ambayo yamekuwepo tangu jadi. |

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| C.B.S: | Colombia broadcasting system- Nembo ya mauzo iliyotumiwa na taifa la Colombia kuuza muziki katika mataifa mbalimbali. |
| E.M.I: | Electro-magnetic interferences – Shirika la Uingereza lililokuwa likirekodi muziki nchini Kenya. |
| M.C.S.K: | Music copyright society of Kenya. |

# YALIYOMO

**IKIRARI** ..................................................................................................... **ii**

**TABARUKU** ..................................................................................................... **iii**

**SHUKRANI** ..................................................................................................... **iv**

**MAELEZO YA ISTILAHI** ..................................................................................... **v**

**MAELEZO YA VIFUPISHO** ................................................................................ **vi**

**YALIYOMO** ..................................................................................................... **vii**

**IKISIRI** ..................................................................................................... **xi**

**ABSTRACT** ..................................................................................................... **xii**

**SURA YA KWANZA** ......................................................................................... **1**

**UTANGULIZI** ..................................................................................................... **1**

1.0 Usuli wa mada ............................................................................................. 1

1.1 Suala la utafiti ............................................................................................. 2

1.2 Malengo ya utafiti ........................................................................................ 3

1.3 Maswali ya utafiti ......................................................................................... 3

1.4 Sababu za Kuchagua Mada .......................................................................... 4

1.5 Upeo na mipaka ya utafiti ............................................................................. 5

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........................................................................ 6

1.7 Msingi wa Nadharia .................................................................................... 10

1.7.1 Nadharia ya Uhalisia ................................................................................ 10

1.8 Mbinu za utafiti ........................................................................................... 12

1.8.1 Mahali pa utafiti ........................................................................................ 13

1.8.2 Sampuli lengwa ........ 14
1.8.3 Ukusanyaji wa data ........ 14
1.8.4 Uchanganuzi wa data ........ 14
1.8.5 Uwasilishaji wa data ........ 15
1.9 Hitimisho ........ 15
**SURA YA PILI ........ 16**
**MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZILIZOPENDWA ZA KIKUNDI CHA MAROON COMMANDOS NA DAUDI KABAKA ........ 16**
2.0 Utangulizi ........ 16
2.1 Udaku ........ 18
2.2 Ukosefu wa kazi ........ 20
2.3 Kutelekezwa kwa watoto ........ 23
2.4 Ombaomba Mitaani ........ 25
2.5 Uvivu ........ 27
2.6 Mafarakano katika ndoa ........ 30
2.7 Mapenzi ........ 34
2.8 Hitimisho ........ 37
**SURA YA TATU ........ 38**
**MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI KWENYE NYIMBO ZA MAROON COMMANDOS NA DAUDI KABAKA ........ 38**
3.0 Utangulizi ........ 38
3.1 Takriri ........ 39

3.1.1 Takriri Mishororo ........ 39
3.1.2 Takriri fungu ........ 40
3.2 Balagha ........ 41
3.3 Tashbihi ........ 43
3.4 Taashira ........ 44
3.5 Chuku ........ 45
3.6 Methali ........ 46
3.7 Hitimisho ........ 48
**SURA YA NNE ........ 49**
**ULINGANIFU KATI YA NYIMBO ZA DAUDI KABAKA NA MAROON COMMANDOS ........ 49**
4.0 Utangulizi ........ 49
4.1 Mazingira ........ 50
4.2 Utamaduni ........ 52
4.3 Mwingiliano wa Maudhui ........ 55
4.4 Uteuzi wa Lugha ........ 57
4.5 Mtindo wa Usimulizi ........ 59
4.6 Usawiri wa Wahusika ........ 63
4.7 Hitimisho ........ 64
**SURA YA TANO ........ 65**
**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO ........ 65**
5.0 Utangulizi ........ 65
5.1 Muhtasari wa Utafiti ........ 65

5.2 Matokeo ya Utafiti ..... 67

5.3 Matatizo ..... 69

5.4 Mapendekezo ..... 70

**MAREJELEO ..... 72**

**VIAMBATISHO ..... 76**

Kiambatanisho I: Nyimbo ..... 76

Kiambatanisho II: Hojaji ..... 96

## IKISIRI

Utafiti huu umelenga kuhakiki **Maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili: Mtazamo linganishi wa Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos**. Nyimbo hizi ziliimbwa katika kipindi cha kati ya mwaka wa 1960 hadi 1990. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii hutumika katika fasihi kuelezea jinzi hali ilivyo katika jamii kiuchumi, kijamii, kisiasa na kitamaduni. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na nyanjani. Mtafiti alipitia kanda za santuri zilizohifadhi nyimbo hizo na pia kusoma makala mengi kuhusu mada hii ili kukusanya data toshelevu. Data iliyokusanywa ilirekodiwa na kuchunguzwa kuambatana na malengo na maswali ya utafiti. Ripoti ya utafiti huu imewasilishwa katika sura tano. Sura ya kwanza inahusu mada ya utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia ya utafiti. Sura ya pili imefafanua maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Sura ya tatu imebainisha namna matumizi ya tamathali za usemi zimechangia katika ujenzi wa maudhui kwenye nyimbo husika. Sura ya nne imetupatia ulinganifu uliopo kati ya waimbaji hawa wawili. Sura ya tano imetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya tafiti za baadaye. Kazi hii itakuwa muhimu sana kwa watafiti wa fasihi na waimbaji wa sasa na wale wa baadaye katika kuboresha viwango vya utunzi wao.

## ABSTRACT

The research intended to investigate **themes in popular Swahili songs: A comperative approach of Daudi Kabaka and Maroon Commndos group.** The songs were sang between the year 1960 and 1990. The research was guided by realism theory. The researcher went through recorded songs stored in round discs. Selected literary materials were also read for the purposes of getting data. The collected data was recorded and analysed guided by the research questions and objectives. The report was presented in five chapters. Chapter one includes the study topic, research questions, objectives of the study, justifications for the study, scope of the study, literature review and theoretical framework. The second chapter analyses themes in Daudi Kabaka and Maroon Commandos group songs. Chapter three examines how language use has aided in making the themes come out clearly. The fourth chapter examines the comparisons found between the works of the two artists. The fifth chapter includes summery, conclusion and recommendations for further research. This research will benefit other literary scholars and current artists to make their work better.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa mada

Nyimbo ni mojawapo ya vipera vya ushairi simulizi. Hupangwa kwa muwala wenye wizani na tungo hizi huimbwa na aghalabu huwa na muundo wa kishairi. Finnegan (1977), anasema nyimbo ni chombo mwafaka cha fasihi simulizi kinachoongoza jamii ili kufikia malengo ya ufanisi. Ili wimbo uvutie hadhira na kudumu, unahitaji kuwa na muundo wenye uzito wa lugha na unaojenga taswira inayoathiri fikra za wapokezi wake. Nyimbo hutungwa katika kipindi fulani cha wakati. Baadhi ya nyimbo hizo hufifia na zingine hudumu kwa vipindi tofauti na huwa zinapendwa na hadhira au vizazi vya vipindi hivyo.

Nyimbo zilizopendwa za Kiswahili zimeweza kuvutia hadhira kubwa sana kwa sasa. Kulingana na Schumann (1994), asili ya muziki haijulikani. Brandel (1959) na Akuno (1999), wameeleza kuwa muziki ni zaidi ya sauti ambazo huimbwa na kuchezwa. Muziki ni muhimu sana katika kuelezea historia ya jamii, imani na itikadi zake. Kwa sababu hii, nyimbo ni zao la mazingira ya jamii na hufungamana sana na muktadha wa mazingira ya mtunzi na jamii kwa jumla.

Ni katika muktadha huu ambapo nyimbo za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos zimeteuliwa kwa maksudi ili maudhui ya nyimbo hizoyadhihirishe mshikamano wake na mazingira ya utunzi wao. Muziki huu umeweza kuwafikia wengi hasa kupitia vyombo vya habari na nyimbo kama fasihi zimetumika kuonyesha hatua mbalimbali ambazo jamii imepitia tangu mwaka wa elfu moja mia tisa na sitini.

Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya utafiti huu ili kutathmini nyimbo hizi ambazo zilitungwa katika vipindi tofauti vilivyopita na jinsi nyimbo hizi zimeweza kufaa jamii ya baadaye.

**1.1 Suala la utafiti**

Nyimbo ni tungo za fasihi ambazo hufuata mtindo wa kishairi na hutekeleza dhima maalumu katika jamii. Nyimbo ni za aina mbalimbali mathalan za kisiasa, kidini, kiuchumi na za kijamii. Nyimbo ambazo zimehakikiwa katika utafiti huu ni zile zilizopendwa za Daudi Kabaka na na kikundi cha Maroon Commandos na ambazo zimehifadhiwa kwenye santuri, kaseti na katika vifaa vinginevyo vya kielektroniki. Nyimbo hizi zilitungwa katika kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni nchini Kenya. Utunzi wao ulijikita katika mahitaji maalumu ya jamii. Pia, licha ya kwamba nyimbo hizo zilitungwa miaka mingi iliyopita, bado zina hadhira yake na zinapendwa na hadhira husika ambayo inazidi kupanuka kila siku bila kubagua wazee na hata vijana.

Maudhui ya nyimbo hizi yana umuhimu wake kwa vizazi vya zamani, vya sasa na vya baadaye kwani zinahifadhi utamaduni wa wakenya. Maudhui katika tungo hizo japo zilitungwa miaka mingi iliyopita yanajitokeza kwa sasa inavyo fafanuliwa katika suea ya pili. Nyimbo nyingi ziliwasilishwa kwa lugha ya Kiswahili. Hii ndio lugha inayoeleweka na wakenya wengi na jamii pana ya waswahili. Mshikamano wa maudhui na tamaduni za jamii halisi unaowakilishwa na nyimbo hizi umechochea aina hii ya utafiti. Nyimbo hizi zilichochea utafiti huu ili maudhui na mazingira ambamo zilitungwa yaweze kubainishwa na kuchanganuliwa kwa kina. Vilevile, nyimbo hizi zinachezwa katika sehemu nyingi za burudani kama vile kwenye mabaa ya mijini na mashambani na wateja huzipenda sana.

Idhaa mbalimbali za redio kama vile Kenya broadcasting cooperation zimeratibia muda wa kuzicheza na mapokezi yake ni mazuri kwa hadhira lengwa. Sababu hizi zilichochea aina hii ya utafiti.

## 1.2 Malengo ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafutayo:

(a) Kufafanua maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos.

(b) Kuonyesha namna tamathali za usemi zilivyochangia katika uwasilishaji wa maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Maroon Commandos na Daudi Kabaka.

(c) Kufafanua ulinganifu uliopo kati ya nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na Maroon Commandos.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

(a) Je, maudhui yanayojitokeza ni yapi katika nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos?

(b) Matumizi ya tamathali za usemi yamechangia vipi katika uwasilishaji wa maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Maroon Commandos na Daudi Kabaka?

(c) Je, kuna ulinganifu gani kati ya nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na Maroon Commandos?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Nyimbo kama tungo zingine za fasihi simulizi zinahitaji ubunifu wa hali ya juu ili zikubalike na hadhira lengwa. Sababu kubwa ni kwamba kuna ushindani mkubwa katika fani hii na kazi ambazo haziwezi zikahimili ushindani huu hufifia na hata kufa. Kunazo sababu mbalimbali zilizochochea uteuzi wa mada hii.

Jambo la kwanza ni maudhui yanayowasilishwa na nyimbo hizi. Dhima kuu ya kazi za fasihi ni kuwasilisha ujumbe kwa njia inayofaa na inayoeleweka kwa urahisi na hadhira lengwa. Nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na Maroon Commandos zimeweza kudhihirisha viwango vya juu katika kuifikia hadhira na kutimiza mahitaji yao. Haya yanapigwa jeki na uteuzi wa lugha ya Kiswahili; lugha inayotumiwa katika afrika mashariki jambo linalobainisha usanifu wa watunzi hawa. Usanifu huu uliwakweza wasanii hao katika nyakati zao na kazi zao zimedumu kwa vipindi tofauti tofauti.

Jambo la pili ambalo limechochea uchaguzi wa mada hii ni kuwa, nyimbo hizi zinatumika sana katika vyombo vingi vya mawasiliano kama vile redio na kwenye simu za mkono kama *"Skiza Tunes"*. Vilevile, wasanii wa miaka ya 2000 wameanza kuziimba upya. Kutumika kwake kunabainisha wazi kuwa zinapendwa jambo ambalo limefanya watu wengi kwa sasa kuanza kuzienzi nyimbo hizi. Aidha, matumizi haya ni dhihirisho kuwa ujumbe unaowasilishwa na nyimbo hizi una muumano na hali halisi ya maisha ya kila siku na mdundo wake husalia nyoyoni za wasikilizaji.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuwa nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za wasanii hawa zimefanyiwa utafiti mchache na kuna haja ya kuziangazia kwa kina. Licha ya kuwa nyimbo kama fasihi simulizi yoyote ile zina dhima mbalimbali, suala la uhalisia

linalowasilishwa na nyimbo hizi haliwezi kupuuziliwa mbali na jamii yoyote ile. Utafiti huu umechangia pakubwa katika kubainisha utamaduni wa wanajamii, mabadiliko yake na mielekeo yao hasa kuhusu maisha jinsi yalivyo.

Aidha, kuna utengano wa kijamii kati ya vijana na wazee unaoletwa na mitindo tofauti ya nyimbo kati ya zile za sasa na za zamani. Nyimbo zilizopendwa zina hadhira yake sasa ambayo inazidi kupanuka jambo ambalo lahitaji kufanyiwa utafiti ili kubainisha sababu hasa za ongezeko la hadhira yake.

**1.5 Upeo na mipaka ya utafiti**

Nyimbo zilizopendwa za Kiswahili ni nyingi mno. Aidha, kuna aina mbalimbali za nyimbo zinazozungumzia maswala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Watunzi wa nyimbo zilizopendwa na bado zinapendwa ni wengi sana nchini Kenya kama vile Fundi Konde, Fadhili Williams, Freshley Mwamburi na Kakai Kilonzo. Utafiti huu umejifunga kwenye nyimbo za Daudi Kabaka zikiwemo zile alizoshirikisha wasanii wenzake kama vile John Nzenze na Jacob William Maunda. Nyimbo zake zilizoteuliwa kwa utafiti huu ni*: Shauri moyo twist, pole musa, taabu ni kwa mwanamume, msichana wa elimu, kabaka says viwete, safari tanganyika na vijana wa mjini*. Pia, nyimbo za kikundi maarufu cha Maroon Commandos zimetumika. Zile zilizoteuliwa ni: *Dawa nimuone hani, usiniambie unaenda, ewe sofia, riziki, uvivu, dada mdaku na Kristina dada.*

Waimbaji waliotajwa hapo juu wameteuliwa kwa maksudi. Ngugi, P. (2000) anasema kuwa umaarufu wa nyimbo zilizopendwa unatokana na sababu kuwa ziliimbwa kwa

lugha ya kiswahili ambayo ni lugha inayofahamika na wengi a frika mashariki na inaeleweka na hadhira pana.

Nyimbo hizo zinachezwa katika vyombo vya habari nchini na hata ughaibuni kama vile idhaa za redio za British broadcasting cooperation (BBC), voice of america (VoA) na deutchewelle (DW) ya Ujerumani. Nyimbo hizo zilianza kuimbwa kati ya miaka ya 1960 na 1970 mtawalia. Hiki ni kipindi cha harakati za kujinyakulia uhuru nchini Kenya na changamoto za baada ya uhuru zilikuwemo. Hivyo, utafiti huu umehakiki maudhui ya nyimbo hizi, mshikamano na mazingira ambamo zilitungwa na uhalisia wake katika jamii kwa ujumla.

**1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Wataalamu wameshughulikia aina mbalimbali za nyimbo kama vile za arusi, nyimbo za watoto, nyiso, vita, wawe, kimai, densi pamoja na maudhui yake. Utafiti huu umeshughulikia nyimbo za Kiswahili zilizotungwa katika kipindi cha mwaka wa 1960 hadi 1980, zikahimili ushindani katika fani ya ubunifu na umaarufu wake ukadumu mpaka sasa. Hii ndio sababu jamii kwa sasa huziita nyimbo zilizopendwa na utafiti huu ulilenga kuzitumia ili kubainisha maudhui yanayowasilishwa na nyimbo zenyewe. Nyimbo ni kipera cha ushairi simulizi. Imebainika kuwa nyimbo huwa na athari kubwa zaidi kwa jamii kuliko kipera kingine chochote. Hii ni kwa sababu, nyimbo huibua hisia za namna fulani moja kwa moja na ndizo hutumika kwa wingi zaidi kupasha ujumbe.

Wataalamu ambao wameshughulikia mada ya nyimbo ni wafuatao:

Bebey (1975), alishughulikia nyimbo za Kiafrika kwa ujumla huko Kameruni. Alisema kuwa nyimbo hizi japo zina uzuri wake hazitambuliwi ng'ambo. Nyimbo hizi ni za

kijumla sana na hakuzama kwa wasanii mahususi. Alibainisha kuwa umuhimu wa nyimbo ni kupambanua maisha ya wanajamii. Mtafiti amepingana naye kwani nyimbo za kiafrika kwa wakati huu zinakubalika kote ulimwenguni. Mtafiti ameeleza zaidi jinsi nyimbo zilizopendwa ni muhimu katika kupigia mfano mazingira, utamaduni na maisha ya wanajamii katika muktadha halisi.

Chiuri (1984) pia alifanya utafiti wa nyimbo za Joseph Kamaru. Alijaribu kugawa nyimbo za Kamaru katika vikundi vitatu. Alizigawa katika makundi ya kisiasa, mapenzi na jamii. Alipeleleza namna Kamaru alivyotumia lugha kuendeleza nyimbo alizotunga. Utafiti huu umetufaa kwa sababu kipengele cha lugha ni muhimu katika kubainisha uhalisia wa nyimbo zilizopendwa. Tofauti iliyoko ni kuwa Chiuri alishughulikia maudhui kwa ujumla kutoka kwa msanii mmoja lakini utafiti huu umelinganisha maudhui ya wasanii wawili wa kipindi kimoja.

Kabira na Mutahi (1988) walitafiti na kuandika kitabu kuhusu nyimbo katika jamii ya wagikuyu hasa nyimbo za vijana kuhusu mungu wanayemwamini. Maudhui katika nyimbo hizi yalihusu mateso waliyoyapata kutoka kwa mkoloni katika harakati za kupigania uhuru. Pia, waliandika kuhusu nyimbo za kusifu mashujaa wao kama vile Mzee Jomo Kenyatta. Hawakushughulikia maudhui ya nyimbo zilizopendwa za Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti wao ni tofauti na wetu. Pia, nyimbo zao zimejikita katika mazingira finyu ya jamii moja ilhali utafiti wetu umehakiki nyimbo za jamii pana ya watu wanaotumia lugha ya Kiswahili.

Ntaragwi, M. (1990) alifanya utafiti wake kuhusu maudhui yanayojitokeza katika nyimbo za Ramadhani Ongala. Hufahamika kama Remy Ongala katika uwanja wa muziki na

akajipa lakabu ya Sura mbaya. Ntaragwi alionyesha namna nyimbo zinavyoyapa maudhui uzito kuliko fani. Nia yake ilikuwa ni kubainisha namna maudhui ya utetezi wa jamii yanavyojitokeza katika nyimbo za Ramadhan na jinsi ambavyo maudhui hayo yalikuwa na uhalisia katika jamii. Kwa sababu maudhui hufungamana na mahitaji ya jamii, kazi ya Ntaragwi imetufaa sana katika kuangazia mazingira ambamo nyimbo za Daudi Kabaka na Maroon Commandos yamejikita. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa umejikita katika utetezi wa jamii bali wetu umehakiki maudhui ya nyimbo zilizopendwa kwa ujumla.

Katika tasnifu yake, King'ei (1992) alifanya utafiti wa kina kuhusu nafasi ya nyimbo za taarabu katika lugha, utamaduni na mawasiliano katika jamii ya waswahili kuanzia mwaka wa 1963 hadi 1990. Alibainisha historia ya nyimbo za taarab, maendeleo yake afrika mashariki pamoja na mtindo na lugha katika nyimbo hizo. Taarabu ni neno ambalo hutumiwa kuashiria muziki wa Kiswahili uimbwao na kuchezwa katika pwani ya afrika mashariki. Aidha katika kazi yake, King'ei aliangazia maudhui ya kijamii na ya kitamaduni katika nyimbo za taarab. Alibainisha namna watunzi wa nyimbo za taarab wanavyothamini ule usanifu wa kiisimu na ule wa kisanaa. Utafiti huu umetufaa kwani umejadili umuhimu wa usanifu katika utunzi wa nyimbo. Nyimbo za taarab hupitisha masuala mengi ya kijamii kwa hadhira yake jambo ambalo ndicho kiini cha utafiti huu.

Wambua, S. (2001) alifanya utafiti wake kuhusu mtindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Alibainisha kwamba uteuzi wa lugha katika uwasilishaji wa ujumbe ndilo jambo muhimu sana katika tungo zozote zile za kazi ya fasihi. Aliweka wazi uhusiano uliopo katika uteuzi wa lugha yenye ubunifu na maudhui katika nyimbo

husika. Nyimbo ambazo zilishughulikiwa na Wambua ni za densi na zilitungwa katika kipindi kinachoangaziwa kwenye utafiti huu. Hii inamaanisha kwamba utafiti huu ulitufaa kwani nyimbo hizi zimesheheni vipengele vya kimaadili ambavyo vimetumika katika kufanikisha utafiti wetu kwani vipengele vya kimaadili ni moja wapo ya maudhui katika kazi za fasihi.

Ngure (2003) alisema kuwa ingawa nyimbo hutumiwa kwa burudani, haziimbwi kwa kufurahisha tu bali kuna jambo zaidi linalowasilishwa. Alisema kwamba nyimbo katika ushairi simulizi hubeba fikra, falsafa na hisi nzito za msanii anazodhamiria kuzipitisha kwa hadhira yake. Nyimbo zinahusiana na maisha, utamaduni, siasa, dini, elimu na mazingira ya nje na ya ndani ya mwanadamu. Maoni ya Ngure yanahusu jinsi nyimbo huwasilisha maisha ya binadamu kwa ujumla. Utafiti huu ni tafauti na wetu kwa sababu utafiti huu ulijifunga kwenye yale mambo yanayofanya nyimbo hizi zipendwe kwa kipindi kirefu na hadhira yake kuzidi kupanuka.

Malenya, (2008) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha na jazanda katika nyimbo za Jacob Luseno. Alisema kuwa matumizi ya lugha kitamathali hufanikisha kazi ya fasihi kama vile nyimbo. Malenya amebainisha usanii wa Jacob Luseno na jinsi alivyotumia lugha na jazanda na jinsi ambavyo msamiati wake unavyoafikiana na vipindi vya utawala nchini Kenya. Usanifu huuumechangiapakubwa katika uchanganuzi wa matumizi ya lugha katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wetu umezama na kupanuka zaidi hadi kwa wasanii wengine nchini na jinsi maudhui kwenye nyimbo hizo yanavyopigia mfano maisha halia ya binadamu.

Mue, (2013) alifanya utafiti wake kuhusu maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za injili za Rose Muhando. Utafiti wake ulijikita katika muktadha wa nyimbo za dini ya kikristo na wa kijamii. Anaonyesha jinsi nyimbo huibua mihemko na hisia za watu. Hisia hizi huongozwa na mielekeo ambayo yaweza kuwa hasi au chanya. Pia, alibainisha namna nyimbo hizi zinaweza kutumiwa kumwongoza mwanadamu katika matendo yake duniani. Utafiti huu umejikita sana katika dini. Hata hivyo, ulifaa kwa sababu dini huongoza mwanadamu na ukamilifu wa mwanadamu hudhihirika kupitia maisha anamoishi na mwongozo wake hupatikana katika imani. Pia kuna uwiano mkubwa baina ya dini na mitazamo ya watu kuhusu imani na tamaduni zao. Haya husaidia watunzi kama wanajamii kuibua maudhui yanayofungamana na mazingira ya hadhira lengwa.

## 1.7 Msingi wa Nadharia

Kuna nadharia moja mwafaka ambayo iliongoza utafiti huu. Nadharia hii ni ya **Uhalisia.** Hii ni kwa sababu kulingana na nadharia hii, mwandishi hudhamiria kuonyesha ukweli katika jamii jinsi ulivyo.

### 1.7.1 Nadharia ya Uhalisia

Uhalisia ni dhana inayotumika katika fasihi kuelezea hali ilivyo katika jamii kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Hii inamaanisha kuwa nadharia hii hujikita katika utoaji wa picha halisi ya maisha ya binadamu. Hivyo basi watunzi wa nyimbo za kihalisia huandika juu ya mambo ambayo yalitendeka na yanaendelea kutendeka katika jamii ya sasa.

Kulingana na Lukacs (1972), waandishi wa karne ya kumi na nane walishughulikia tu masuala yaliyozikumba jamii zao. Alielezea kwamba mwanauhalisia wa kweli ni yule anayepata suluhisho la tatizo la kimsingi la wakati wake. Boyles na Swales (1986),

wanaeleza jinsi uhalisia unapaswa kueleza vitu jinsi vilivyo. Hawa walikuwa wakimrejelea Proust ambaye aliandika kuhusu kile ambacho kingeonyesha umuhimu wa nafsi na aliyoyapitia mwanajamii. Maoni haya yanaoana na maudhui katika nyimbo za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos na maisha ambayo jamii imepitia. Mbatia, (2001) anasema kuwa uhalisia ni tapo la uandishi uliozuka karne ya kumi na nane kule ulaya na kusambaa ulimwenguni kote. Aliendelea kusema kuwa ukweli wa maisha ya binadamu hupatikana katika maisha ya kila siku. Hivyo basi, walijikita katika mazingira halisi ya jamii na kuyasawiri jinsi yalivyo bila kupotosha wala kutia chumvi.

Kulingana na Wafula na Njogu (2007), uhalisia ndio nadharia muhimu zaidi kuwahi kutokea katika karne ya kumi na tisa na ishirini. Walikuwa wakizungumzia uhalisia katika fasihi ya kimagharibi hasa ulaya. Walidai kwamba uhalisia ulitokana na matatizo yaliyokuwa yakiwakabili watu; matatizo ambayo yaliwafanya waanze kuutuhumu ulimbwende. Matamanio ya kilimbwende yalikuwa ya kinjozi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu nyakati hizo.

Hegel katika kitabu chake *Aesthetic* anaeleza kuwa kazi ya kifasihi inapaswa kuwasilisha ulimwengu wa maisha ya jamii kwa sababu mhusika au wahusika hutenda mambo kulingana na jinsi wanavyochochewa na hali ya kisaikolojia inayowazunguka. Flaubert alidai kwamba mtu hufikiria kwa kichwa chake, hafikirii kwa moyo wake. Hapa alikuwa akilaani dhana iliyowaongoza walimbwende katika utungaji wao. Kulingana na Rene Welleck katika jarida la *Neophilologus*, dhana ya uhalisia ilianza kutumika mapema takribani mwaka wa 1790.

Kulingana na mitazamo ya wasomi hawa, dhana ya uhalisia imekuja kuhusishwa na miktadha tofauti. Kwanza ni kutathmini hali au halia ya maisha jinsi yalivyo.Pili ni kuwa kazi ya fasihi ama sanaa inapaswa kuonyesha maisha ya binadami jinsi yalivyo.

Nadharia ya uhalisia ina mihimili ifuatayo:

(a) Uhalisia ni nadharia inayotumika kulinganisha fasihi na hali halisi katika jamii. Mhimili huu umetumika kuonyesha picha halisi ya jamii inayozungumziwa na waimbaji wa vikundi vya Maroon Commandos na Daudi Kabaka bila kuidunisha wala kuipigia chuku.

(b) Dhima ya mwandishi ni kuonyesha jamii jinsi ilivyo. Kama ilivyo katika nyimbo za Daudi Kabaka na Maroon Commandos, watunzi hawa walifaulu kuonyesha ukweli wa maisha ya binadamu katika hali zote mara tu baada ya uhuru. Mhimili huu ulifaa katika kupigia mfano maisha halisi ya wanajamii katika mazingira wanamoishi.

(c) Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida na wanaopatikana katika jamii halisi, huyachunguza na kusimulia maisha yao, tajiriba zao na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Utafiti huu umejifunga katika maudhui ya nyimbo za Daudi Kabaka na Maroon Commandos kwa hivyo umeongoza katika kufafanua mambo halisi yanayopatikana katika jamii.

## 1.8 Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na nyanjani. Maeneo yaliyotembelewa ni miji ya Nairobi, Machakos na Mombasa na vitongoji vya miji hii mikubwa.

Katika utafiti wa nyanjani, maswali ya hojaji yalipewa wasikilizaji na wapenzi wa nyimbo hizi kujaza. Mbinu hii ilikusanya data kuhusu nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos zenye maudhui yanayooana na utamaduni wa wakenya. Utafiti huu ulihusisha watu walio na umri wa miaka kumi na minane na zaidi. Hii ni kwa sababu wana tajriba ya kutosha kuhusu nyimbo kwa hivyo data kamilifu ilikusanywa. Usambuliaji huu ulihusisha watu kumikumi wenye umri tofauti tofauti katika maeneo hayo. Maswali ya hojaji walipewa na kujaza. Baadhi ya wasanii walioimba na vikundi vinavyorejelewa wangali hai kwa hivyo mahojiano pia yalitumika ili kufanikisha kazi hii. Data ilihusu umuhimu, umaarufu na ufaafu wa nyimbo hizo kwa sasa.

Pia, utafiti huu ulifanywa kwenye maktaba. Nyimbo nyingi za Daudi Kabaka na Maroon Commandos zimehifadhiwa katika maktaba za muziki kwenye santuri na vifaa vingine vya kielektroniki. Nyimbo hizo zilisikizwa na kuteuliwa kwa minajili ya utafiti huu. Pia tasnifu nyingi kuhusu nyimbo zipo maktabani na zilisomwa kwa kina ili kuboresha utafiti huu. Tasnifu na kazi nyinginezo zilichangia katika kutathmini yaliyoandikwa kuhusu nyimbo hizi ili kujaliza udhaifu uliopo kwenye tafiti hizo na hata kuziboresha kwa kutoa mchango wa ziada.

### 1.8.1 Mahali pa utafiti

Ili kufanikisha utafiti huu, maktaba pekee haikutosha. Mtafiti alilazimika kutembelea maeneo mbalimbali ya burudani mijini Nairobi, Machakos na Mombasa ambako nyimbo hizi huchezwa katika maeneo hayo teule ya burudani. Hii ni miji mikubwa nchini na ilitosha kuteuliwa kama sampuli ili kuwakilisha tamaduni mbalimbali. Katika miji hii,

sehemu zilizotembelewa ni vilabu teule vinavyocheza nyimbo hizi. Pia, mtafiti alitembelea maeneo ya vitongoji katika sehemu zizo hizo ili kupata maoni kamili ya mijini na vitongojini kuhusu nyimbo hizi. Sehemu hizi ni maksudi kwani ni miji inayohifadhi watu wenye tamaduni tofauti. Aidha, baadhi ya bendi zingalipo kwa hivyo vinara wao walihojiwa na maoni yao kufanikisha utafiti huu.

### 1.8.2 Sampuli lengwa

Sampuli lengwa hapa ni nyimbo za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Uteuzi wa wasanii hawa ulikuwa wa kimaksudi kwani maudhui ya nyimbo zao yanarejelea uhalisia wa maisha ya wanajamii. Mtafiti ameteua nyimbo saba kutoka kwa kila mmoja ambazo zimechanganuliwa kufanikisha utafiti huu.

### 1.8.3 Ukusanyaji wa data

Katika ukusanyaji wa data, nyimbo za Daudi Kabaka na bendi ya Maroon Commandos za kipindi husika zilisikizwa na kunakiliwa. Baadaye uhakiki wa nyimbo hizo ulifanywa huku suala la maudhui likitiliwa maanani. Mahojiano na maswali ya hojaji yaliyojazwa vilevile yalitumiwa kutathmini ufaafu wa nyimbo hizi katika jamii halisi.

### 1.8.4 Uchanganuzi wa data

Baada ya data kukusanywa, ilipangwa na kuainishwa kulingana na malengo ya utafiti. Uchanganuzi uliongozwa na malengo, maswali, pamoja na mihimili ya nadharia ya uhalisia. Ujumbe ulio muhimu ndio uliotumika ili kukidhi mahitaji ya mada kwa sababu dhima kuu ya uchanganuzi wa data ni kujibu maswali ya utafiti na kutathmini nadharia tete kama ina utoshelevu au la.

### 1.8.5 Uwasilishaji wa data

Kama ilivyo katika kazi za fasihi zozote zile, matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Ufafanuzi wa kina umetolewa kuhusu maudhui pamoja na mtindo wa uwasilishaji lugha kwenye nyimbo hizi. Ulinganifu uliopo kati ya vikundi vya waimbaji hawa umewasilishwa.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imefanikiwa kueleza msingi wa utafiti huu pamoja na suala la utafiti na malengo yake yamewekwa wazi. Aidha, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti na yaliyoandikwa kuhusu mada yamefafanuliwa. Mengine ambayo yamezungumziwa ni pamoja na msingi wa nadharia, nadharia ya uhalisia, mbinu za utafiti, mahali pa utafiti, sampuli lengwa, ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Hatua hizi zote zimeupatia mwelekeo utafiti huu ili kuhakikisha kuwa kuna utoshelevu. Sura inayofuta imezungumzia kuhusu maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za Daudi Kabaka na Maroon Commandos.

# SURA YA PILI

# MAUDHUI KATIKA NYIMBO ZILIZOPENDWA ZA KIKUNDI CHA MAROON COMMANDOS NA DAUDI KABAKA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia uchanganuzi wa maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za bendi ya Maroon Commandos na Daudi Kabaka.

Maroon Commandos ni kikundi cha wanamuziki kutoka Kenya. Hii ni bendi ya wanajeshi ambayo makao yake makuu ni kambi ya kijeshi ya Lang'ata, jijini Nairobi. Bendi hii hucheza sana muziki ambao mtindo wake hufahamika sana kama benga na rhumba; mitindo ambayo ni maarufu sana katika kanda la afrika mashariki. Aghalabu nyimbo zao huziimba wakati wa sherehe za kitaifa. Bendi hii ilianzishwa mwaka wa 1970 na iliongozwa na Habel Kifoto. Walitoa wimbo wao wa kwanza *"Emily"* mwaka wa 1971. Mwaka wa 1972, waimbaji hawa walipatwa na ajali ya barabarani na baadhi yao wakaaga dunia. Hali hiyo ilifanya bendi hii kuingia katika kipindi cha ukimya kwa miaka mitano. Mwaka wa 1977 waliimba wimbo *"Charonyi ni wasi"* ambao uliandikwa kwa lugha ya Kitaita kwenye albamu "Riziki haivutwi". Bendi hii iliundwa kwa madhumuni ya kutumbuiza wanajeshi wenzao kambini.

Tangu kuanzishwa kwake, bendi hii imepitia mabadiliko mengi ya uongozi. Habel Kifoto alistaafu jeshini na kuchanguliwa mwenyekiti wa bodi inayosimamia muziki nchini ya Music Copyright Society of Kenya (M.C.S.K) hadi 2009. Wengine waliongoza bendi hii ni Laban Ochuka, Diwani Nzaro na David Kombo. Ijapokuwa wengi ni wanaume, kuna wanawake wachache ambao pia huimba kama vile Chepchumba Tanui na Barbara

Chepkoech au Waridi. Bendi hii imekuwa ikiimba nyimbo zinazozugumzia kuhusu maisha ya watu jinsi yalivyo. Mwaka wa 2008, walitunga wimbo "*Kenya unite*" (tuungane wakenya), unaozungumzia kuhusu vita vilivyotokea baada ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 hadi 2008 nchini Kenya.

Kwa sasa, kikundi hiki kinawakubalia wanamuziki wengine ambao si wanajeshi kujiunga nao. Mwanzilishi wa bendi hii habel Kifoto aliaga dunia Julai 2011, Nairobi.

Daudi Kabaka ni mtunzi, msanii na mwimbaji wa Kenya aliyezaliwa mwaka wa 1939 na kuaga dunia mwaka wa 2001. Yeye kama wanamuziki wengi nchini alicheza aina ya muziki wa "Twist" ambao ndio mtindo maarufu afrika mashariki. Aliishi katika vipindi muhimu sana nchini Kenya kati ya vita vikuu vya pili vya dunia, harakati za kupigania uhuru, baada ya uhuru na hata kushuhudia mabadiliko mengi ya maisha ya wakenya hadi mwaka wa elfu mbili. Nyimbo zake bora zinazojulikana ni pamoja na African *twist, Harambee harambee na Western shilo*. Wimbo wake wa *Harambee harambee* unajulikana sana nchini kwani kwa kiasi kikubwa huonyesha matumainio ya wakenya baada ya ukoloni ili kujenga upya Kenya kwa pamoja.

Daudi Kabaka pia aliweza kushikirikiana na waimbaji wengine kama vile John Nzenze na kutoa nyimbo kama *Masita, Bachelor boy* na *Nyumba za tumbako*. Aliweza pia kushirikiana na Maroon Commandos mwaka wa 1986 na kutoa albamu *'Pesa maradhi ya moyo'*. Hadi kifo chake, alikuwa akitumbuiza katika majumba ya starehe jijini Nairobi na chuo kikuu cha Kenyatta katika tamasha za kila mwaka za kuadhimisha tamaduni mbalimbali chuoni humo. (Culture week)

Maudhui yaliyochanganuliwa yamejikita katika muktadha wa maisha halisi ya jamii. Uchanganuzi huu umeongozwa na nadharia ya uhalisia kama ilivyofafanuliwa katika sura ya kwanza. Malengo ya utafiti yametiliwa maanani katika kuchanganua masuala ya kijamii. Katika uchanganuzi wa nyimbo hizo, maudhui yafuatayo yanajitokeza:

(a) Udaku

(b) Ukosefu wa kazi

(c) Kutelekezwa kwa watoto

(d) Ombaomba mitaani

(e) Uvivu

(f) Mafarakano katika ndoa na mapenzi

**2.1 Udaku**

Udaku ni tabia ya kutafuta na kutaka kujua habari za watu (TUKI 2003). Pia huitwa umbeya. Kulingana na nadharia ya uhalisia, wanauhalisia huchukulia fasihi kama kioo cha jamii. Picha halisi ya jamii huwasilishwa bila kudunisha wala kuipigia chuku. Nyimbo za msanii Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos zimeweza kuizungumzia jamii ambayo baadhi ya watu wamejawa na udukuzi na wamo mbioni kuchunguza mambo ya wenzao katika jamii tunamoishi. Katika wimbo *"Dada mdaku"*, Maroon Commandos wanasema mambo yafuatayo kuhusu dada mdaku.

*Mwenendo wako sio mwema, ewe dada jirekebishe,*

*Mwenendo wako sio mwema, ewe dada jirekebishe,*

*Ya nini kuzururazurura, umefahamika*

*Ya nini kuzururazurura, umefahamika.* (ubeti 1)

Dada mdaku amefahamika kwa kuzururazurura katika nyumba za watu vijijini na kuwavurugia amani yao. Watu wamemjua na wameanza kumkataza kwenda kwao. Hii ni tabia ambayo inajitokeza sana katika jamii na watu hawa huchukuliwa kama watu hatari katika kuharibu na kuvunja nyumba za watu. Waimbaji hawa wanaendelea kusema kuwa:

*Umevuruga nyumba nyingi, na kwetu usije tena*

*Tafuta kijana wa hapo kwenu, awe rafiki yako utulie.*

*Tafuta kijana wa hapo kwenu, awe rafiki utulie.*

*Wana maroon wameshaona mambo yako si mazuri*

*Tabia zako wewe sio nzuri, bora tukueleze waziwazi* (ubeti 2)

Haya yanadhihirisha kuwa udaku kama ulivyo katika jamii nyingi husababisha mafarakano katika jamii. Umbeya haukubaliwi katika jamii. Jamii huchukulia jambo hili kama ambalo husababishwa na ulofa ama kutoolewa kwa wanawake. Dada mdaku anashauriwa aolewe ili atulie, aache kuzurura akitafuta mambo ya wengine ama kuwasha moto katika nyumba za watu. Katika wimbo huu wenye beti nne, mwimbaji anamshauri kuwa atafute mume aolewe ili awe na shughuli za kwake aache mambo ya watu.

Katika wimbo wa Kabaka wa “Safari ya Tanganyika” anasema:

*Usidani nitamuoa mwingine Tanganyika,*

*Hata mimi nikitembea nakuwaza masita,*

*Nifanyeje safari yangu sa itavunjika,*

*Nikoredi baby ni shida sheri kwa safari. { ubeti 2}*

Maneno haya yanatokana na uwezekano kwamba mtu anapoenda katika nchi tofauti wadaku huanza kumpotosha bibi aliyebaki nyuma. Wanamwambia kwamba huko kesha pata mwingine. Haya yanatokana na ukweli kwamba aliyesafiri hapati nafasi ya kurudi nyumbani mara kwa mara

Hivyo basi swala la udaku lipo katika jamii zetu kwa sasa na linachangia katika kuvuruga familia.

**2.2 Ukosefu wa kazi**

Suala la ukosefu wa kazi limekuwa donda sugu katika mataifa mengi ulimwenguni hasa mataifa ya ulimwengu wa tatu. Inafahamika kwamba ili jamii inawiri kiuchumi, wanajamii wenyewe lazima wajihusishe katika shughuli za kiuchumi ambazo zitaleta natija kwao. Nadharia ya uhalisia inasisitiza kuwa dhima ya mwandishi ni kuonyesha jamii jinsi ilivyo. Kikundi hiki cha Maroon Commandos na Daudi Kabaka walifaulu kuonyesha ukweli wa maisha ya binadamu ambayo yamekumbwa na ukosefu wa kazi. Daudi kabaka anasema kuwa yeyote anayekosa kazi hukumbana na taabu zote. Katika wimbo "*Taabu ni kwa mwanamume"*, anasema kuwa anayekosa kazi taabu zote humwandama.

*Ukizaliwa wewe ni kijana,*

*Ukose kazi taabu yote itakupata.*

*ooh darling Marina baby*

*Umeniacha ati sina kazi*

*Ukizaliwa wewe ni kijana,*

*Ukose kazi taabu yote itakupata.* (ubeti 1)

Mtu anapokosa kazi huwa na shida nyingi na hata watu huanza kumwambaa bila kujali uhusiano wa ukoo. Ubeti wa tatu wa wimbo huo unaonyesha jinsi watu wa familia hukukwepa ukiwatembelea kwani unachukuliwa kama mtu ambaye amekuja kuomba usaidizi na mtegemezi.

*Ukienda kuona mtu wa kwenu,*

*Ukitoka wanaanza masengenyo.*

*Ukienda kuona mtu wa kwenu,*

*Ukitoka wanaanza masengenyo.* (ubeti 3)

Katika jamii ya kisasa, kazi si rahisi kupatikana. Mtunzi Daudi Kabaka anasema kuwa wanajamii hujibidiisha kutafuta kazi zozote zile bora afanikiwe. Anauliza katika wimbo huu kuhusu kazi iliyo bora kwani vijana wengi hubagua kazi.

*Huyu kijana kazi gani anataka,*

*Kupeleka ndege ama kupeleka gari*

*Ooh kazi ni ngumu mama*

*Nimetafuta sasa nimeshindwa.*

*Lakini bwana wewe ukumbuke*

*Kazi ya mzungu lazima hutafutwa*. (ubeti 4)

Mtunzi hapa anapitisha ujumbe kwa vijana waache kubagua kazi kwani kazi za ofisini hazipatikani ingawa vijana wengi huwa wanazitafuta kila mara. Kwa hivyo, huu ni wimbo unaoangazia jamii ya sasa iliyo na shida ya ukosefu wa kazi tatizo ambalo ni halia katika mataifa mengi.

Katika wimbo wa wana Maroon wa *"Riziki"* suala la kazi limeangaziwa. Wanasema kuwa;

*Kazana kazana mwana,*

*Na mwisho utafanikiwa,*

*Usiibe wala usinyang'e,*

*Vya kuiba havina Baraka.*

Wimbo huu unaonyesha wazi kwamba bila bidii kazini ufanisi haupatikani. Watunzi hawa wawili wameshughulikia suala nzito la ukosefu wa kazi ambalo limeghubika mataifa mengi.

**2.3 Kutelekezwa kwa watoto**

Malezi ni jambo muhimu katika jamii. Watoto wanapozaliwa wanahitaji kupewa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi, nguo na elimu nzuri. Mambo haya hayawezekani katika mazingira ambamo wazazi huwatelekeza wanao hasa wanapowakimbia na kuwaacha peke yao. Nadharia ya uhalisia hujikita kwenye wahusika wa kawaida ambao hupatikana katika jamii hai. Pia huchunguza na kusimulia kuhusu maisha yao, tajiriba zao na kuonyesha mandhari ya kawaida. Katika maisha tunamoishi, kikundi cha Maroon Commandos katika albamu yao *"Riziki haivutwi"* wanamrejelea mwanamke Sofia. Sofia ni mhusika wa kawaida anayepatikana katika jamii halisi na analaumiwa kwa kuzaa watoto na kuwakimbia huku akiwaacha katika dhiki kubwa. Mwimbaji anashangazwa na vitendo vya Sofia vya kujifungua watoto na kuwatupa tabia ambayo inendelea katika maeneo mbalimbali nchini. Wanasema;

*Sofia eeh Sofia, mwana mama,*

*Sofia umetenda mambo mabaya,*

*Sofia umewacha eeh, watoto wako,*

*Sawa na kuwatupa eeh, watoto wako.* (ubeti 1)

Kitendo cha wanawake hasa wasichana cha kujifungua watoto na kutorokea mijini kimeenea sana katika jamii. Wanamuziki hawa wanamshauri Sofia arudi nyumbani akawaone watoto wake kwani watoto wanapokua huhitaji mapenzi ya mama yao. Wanamwambia kuwa:

*Watoto uliwazaa, kwa nini uwawache?*

*Rudi nyumbani Sofia eeh, aee,*

*Rudi kaone watoto oo,*

*Rudi nyumbani Sofia aee,*

*Rudi kaone watoto oo* (ubeti 2)

Baadhi ya vyanzo vinavyochangia kutoroka huku ni hasira na kutoelewana miongoni mwa wanandoa. Maroon Commandos wanashauri kuwa watu katika asasi ya ndoa hukosana, husameheana na kuendelea kuishi pamoja ili mahitaji ya kimsingi ya watoto yatimizwe. Katika wimbo "*Sofia*", wana Commandos wanashauri kuwa ni jambo la busara kwa mama kurejea kwake na kuwalea wanawe katika ubeti wa tatu na nne.

*Rudi nyumbani Sofia ee…aee,*

*Rudi kaone watoto…*

*Punguza zako hasira aee,*

*Rudi kaone watoto.*

*Watu hukosana kila mara…*

*Wakasameheana ee…*

*Rudi nyumbani Sofia,*

*Rudi kaone watoto wako.* (ubeti 3 na 4)

Suala la utelekezaji wa watoto ni donda sugu katika jamii zetu na wanaotekeleza haya ni viumbe halisi wanaofahamika na wanapatikana katika mazingira na tamaduni za jamii. Maroon Commandos wamedhihirisha haya katika wimbo huu.

Vilevile, Kabaka katika wimbo *“Kabaka says- viwete”* anasema kwamba;

*Kuuliza jamani si ujinga,*

*Bali ni kujua mengi ya ulimwengu.*

*Hawa viwete wetu wasiojiweza,*

*Hupata mtu na kamtoto,*

*Mkikutana njiani sauti ya kamtoto*. [ubeti 1]

Wimbo huu unatokana na ukweli kwamba wapo wanawake wengi wenye ulemavu ambao wamepachikwa mimba na wanaume ambao hutoweka. Wazazi hawa wa kike huachiwa jukumu la kulea peke yao na hii ni changamoto kubwa mtu mlemavu.

**2.4 Ombaomba Mitaani**

Katika mazingira ya mijini, watu wasiojimudu kiuchumi huibua mbinu mbalimbali za kujitafutia riziki. Miongoni mwa njia hizi ni kuombaomba wapita njia. Nadharia ya uhalisia inalenga kuonyesha jamii jinsi ilivyo. Viwete au watu wenye ulemavu mijini ndio wanadhihirisha maudhui haya. Mwimbaji na mtunzi Daudi kabaka katika wimbo “Viwete” anashangaa jinsi viwete hawa ambao huwa wengi mijini huwapata watoto.

*Kuuliza jamani, si ujinga aah,*

*Bali ni kujua mengi ya ulimwengu.*

*Hawa viwete wetu, wasiojiweza,*

*Hebu niambieni hupata mtu na kamtoto.*

*Mkikutana njiani sauti ya mtoto,*

*Yenye huruma saidia maskini.* (ubeti 1)

Walemavu hawa japo hawajiwezi huwa na watoto. Jambo linaloshangaza ni kwamba, je, watoto wawa hawa huwa wamezaliwa na nani? Ni jambo ambalo si geni mijini la watu wenye ulemavu kuonekana wamewapakata watoto wadogo wakiwashughulikia kwa kuwalea. Katika wimbo huu, hili ni jambo linalostaajabisha jamii.

*Nasikitika kuuliza, wasiojiweza*

*Hawa hutungwa mimba na nani nijuwe,*

*Tusaidie maskini, mtoto na mama*

*Lakini huyu mtoto amezaliwa na nani?* (ubeti 3)

Mtunzi huyu anarejelea jamii ambayo suala la maadili limedorora sana. Anashauri kuwa mtu akizaa na kiwete au bubu amchukue mtoto huyo ili akaweze kumlea kwani aghalabu yaaminika kuwa babake mtoto ni mtu anayejiweza. Ujumbe huu unajitokeza katika kipokeo cha wimbo huu.

*Tutasaidia nani mama na mtoto, aeeh mama na mtoto*

*Tukizaa na kipofu, mtu kizaa na kiwete,*

*Mtu kizaa na bubu chukua mtoto.*

*Aeeh mtoto si mjinga, aeeh mtoto si kipofu*

*Aeeh mtoto si kiwete, aeeh mtoto sio bubu.* (korasi)

Hata hivyo, wengine wanaombaomba mitaani huwa walaghai kama anavyosema msanii Daudi Kabaka. Wengine hulewa pombe na unapopita mitaani wanasikika wakisema wasaidiwe. Hawa ni matapeli ambao wamo katika jamii na wanahitaji kuchukuliwa hatua.

*Wanaume maskini huomba njiani,*

*Saidia maskini akishalewa pombe,*

*Mtu mwenye shida zake sio kulewa pombe,*

*Tembea kila taoni wakati wa usiku,*

*Maskini wanalala varandani za maduka.* (ubeti 3)

Katika mazingira halisi, kuombaomba mitaani kumeongezeka sana. Kuna wale halali na wengine walaghai ambao wanahitaji kuchukuliwa hatua kwani ni matapeli. Pia, wengine wana makwao na familia zao huwatumia kama vitega uchumi. Hili ni jambo la kweli katika muktadha wa jamii halisi tunamoishi.

**2.5 Uvivu**

Uvivu ni hali ya kutotaka kufanya kazi. Mwanajamii ambaye ni mvivu huwa mlegevu katika jambo analolifanya. Serikali yoyote ile huhimiza raia wake kujituma kazini ili nchi iweze kuimarika kiuchumi. Imebainika kuwa wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida wanaopatikana katika jamii huku wakijifunga kwenye mandhari

na mazingira ya kawaida. Wimbo wa Maroon commandos *"Uvivu"* ulitungwa mnamo mwaka wa 1971. Wimbo huu ulifungamana na kauli mbiu ya serikali ya Kenya wakati huo ya kupambana na umaskini, ujinga na magonjwa. Ili kufaulu katika kukabiliana na umaskini, kila mwananchi alihimizwa kufanya kazi kwa bidii kwani uvivu ndio adui mkubwa kwa ujenzi wa taifa. Wanamaroon wanasema kuwa:

*Uvivu ni adui mkubwa,*

*wa ujenzi wa taifa,*

*kwani ndicho kiini hasa,*

*kisababishacho njaa.* (ubeti 1)

Wimbo huu unahimiza kila mtu katika jamii arauke mapema asubuhi na kuelekea katika sehemu zao za kufanyia kazi. Kilimo ndicho uti wa mgongo katika jamii kwa hivyo wanaoenda makondeni wanahimizwa kuchangamkia kazi yao asubuhi na mapema.

*Ewe ndugu yangu wee,*

*amka kumekucha,*

*kamata jembe na panga,*

*twende shamba*. (ubeti 2)

Watoto nao pia hawajasazwa katika kushauriwa ili waepukane na uvivu. Hata nao wanashauriwa waende masomoni kwani elimu ni muhimu sana katika ustawi wa taifa lolote lile. Wanafanyakazi maofisini kama makarani vivyohivyo wanahimizwa kuamka mapema na kwenda kazini mwao.

*Hata wewe mwanangu*

*amka kumekucha*

*kwani hizi ndizo saa*

*za kwenda shule.*

*Hata wewe Karani*

*amka kumekucha*

*kwani hizi ndizo saa*

*za kwenda kazi.*

Wimbo huu kwa jumla unapinga ulegevu kazini kwani wengi wa wanajamii aghalabu hawapendi kuchoka lakini hupenda kufakamia kilichotafutwa na wenzao. Maudhui ya uvivu yanajitokeza sana kwenye jamii na maroon commandos wamefaulu kuonyesha jinsi uvivu ndicho chanzo cha shida katika jamii hasa njaa.

Suala la kazi pia, limeshughulikiwa na Kabaka katika wimbo "*Taabu ni kwa mwanaume"* Anaimba na kusema;

*Ukizaliwa wewe ni kijana,*

*Ukose kazi taabu yote itakupata.*

*Ukizaliwa wewe ni kijana,*

*Ukose kazi taabu yote itakupata.*

Wimbo huu unawaonya wale ambao huamini kwamba kazi ni zile za ofisini. Hawataki kuzumbua riziki kwa kujituma kufanya kazi mbalimbali za kujiajiri.

Katika jamii tunamoishi kwa hivyo, wale wasiotia bidii pamoja na wale wanaobagua kazi huandamwa na shida kila wakati na hili ni jambo halia katika jamii.

**2.6 Mafarakano katika ndoa**

Mafarakano ni mambo yanayosababisha watu kutofautiana katika mahusiano yao au kutoelewana. Jambo hili husababisha kutengana kwa wanajamii ambao mwanzoni walikuwa na mkabala au mlahaka mzuri. Katika ndoa nyingi kwenye mazingira tunamoishi, vurugu zimeweza kutokea kupitia vita, matusi na kila aina ya kutoelewana jambo linalosababisha kuvunjika kwa ndoa. Wanauhalisia hulinganisha fasihi na kioo cha jamii. Jamii ambayo aghalabu imeshindwa kudhibiti mahusiano ya ndoa imeweza kuangaziwa na Daudi Kabaka kwenye wimbo *"Pole Musa"* Katika wimbo huu, mkewe Musa analalamika kwamba amekuwa akivumilia madhila ya kupigwa kama punda kila siku. Kipigo hiki kimeweza kusababisha kufarakana katika familia hii. Katika ubeti wa kwanza wa wimbo huu, Daudi Kabaka amedhihirisha kipigo ambacho wanawake katika ndoa kwa kusema;

*Musa nimevumilia sana,*

*Musa nimevumilia sana,*

*Kupigwa pigwa kama mimi punda,*

*Na sura yangu imeharibika,*

*Na ngumi zako za kila siku Musa,*

*Taabu…taabu…tabu* (ubeti 1)

Ndoa yenye madhila haya husababisha bibi kwenda kwao kama ilivyofanyika kwa mkewe Musa. Mafarakano haya katika jamii hutokana na baadhi ya vitendo ambavyo

havikubaliwi na tamaduni za jamii husika kama vile ulevi wa kupindukia. Hii inadhihirisha kuwa tabia za ulevi zimechangia pakubwa katika kuvuruga asasi za ndoa katika jamii. Pia, vita hivi vimechangia katika kuathiri afya ya mkewe hasa anapopigwa na kuumizwa. Daudi Kabaka anasema haya katika kiitikio cha wimbo huu.

*Kweli Musa, uliponioa,*

*Sura yangu haikuwa na alama hata moja,*

*Nilikuwa na afya nzuri,*

*Nilinona kama ngoima ya kirike.*

(korasi)

*Oyee oyee tafadhali Musa,*

*Tafuta bibi atakayeweza ,*

*Kuvumilia hizo tabia zako,*

*Ukinywa pombe wamunywea yeye,*

*Ukinywa munyeke wamunywia yeye,*

*Poleee poleee.*

Maudhui ya mafarakano katika ndoa yamedhihirika katika jamii nyingi na mara nyingi familia hizi hutengana na kusababisha shida mbalimbali kwa wahusika. Hivyo, jamii inashauriwa iepukane na mambo yanayosababisha kuvurungika kwa ndoa kama vile ulevi wa kupindukia.

Ndoa zenye mafarakano pia huchangiwa na kiwango cha elimu cha mtu binafsi. Imebainika kwamba watu wengi hasa wanawake waliosoma hawataki kuolewa na

wanaamua kuishi peke yao. Daudi Kabaka katika wimbo wake *"Msichana wa elimu"* anashangazwa na msichana mzuri ambaye ana elimu ya kutosha kutoka ughaibuni, lakini hataki kuolewa. Katika wimbo huu, anashauri kuwa miaka ya kuishi huenda haraka sana sawa na siha ya mwanadamu ambayo hubadilika vilevile. Pia anawashauri wasichana hawa waonyeshe mapenzi kwa vijana na waepukane na majivuno na mashauo la sivyo hawatapata wa kuwaoa.

*Msichana wa sura nzuri,*

*Kitu gani kinakufanya usiolewe,*

*Elimu unayo ya kutosha,*

*Hata ng'ambo ukaenda* ukarudi.

*Msichana wa urembo kama wewe,*

*Huonyeshe mapenzi kwa vijana,*

*Ukionyesha majivuno kwa vijana,*

*Utazeeka ukiwa kwenu* (ubeti 1 na 2)

Ndoa pia zimekumbwa na ulaghai. Mtunzi Daudi Kabaka anawasuta wanawake hasa wa mijini kwa kuwadanganya wanaume kwamba hawako kwenye mahusiano ya kimapenzi na wanaume wengine. Hili ni jambo linalijitokeza sana katika jamii na athari zake ni kubwa. Katika wimbo "*Bibi wa Nairobi"*, Daudi Kabaka anashauri wanawake waache ulaghai huu kwani watu huweza kupigana na kuumizana katika ubeti wa kwanza na wa pili.

*Nilikuta bibi wa kwanza Nairobi,*

*Akanipenda nami nikampenda,*

*Nikamwuuliza kama ana bwana,*

*Akanijibu sina hata mpenzi.*

*Tukaenda naye mpaka kwake,*

*Shauri Moyo kwa nyumba za tumbako.*

*Nilipolala kasikia hodihodi*

*Fungueni ni mimi mwenye nyumba*. [ ubeti 1,2]

Kikundi cha Maroon nao katika wimbo wao *"Dawa nimuone hani",* wanasema kwamba;

*Wenzangu nifanye nini, kwani mawazo yamenizidi,*

*Wenzangu nifanye nini, kwani mawazo yamenizidi,*

*Maanake mpaka leo, huteseka juu ya hani,*

*Maanake mpaka leo, huteseka juu ya hani,*

*Tulijaliwa watoto, tulipokuwa nayo mapenzi,*

*Tulijaliwa watoto, tulipokuwa nayo mapenzi,*

*Mpaka leo sijui, hani alipo,*

*Mpaka leo sijui, hani alipo.* (ubeti 2)

Kifungu hiki kinaonyesha kwamba hii ni ndoa ambayo awali ilikuwa ya kupigiwa mfano. Mwanzoni ilijaa mapenzi ya dhati na haikuwa na unafiki wowote. Mumewe hata alimwita mkewe majina mazuri kama vile hani. Katika kipindi hicho hata walijaliwa

watoto. Kilichofanya waachane ni mafarakano katika ndoa na haya ni mambo halia katika maisha ya zamani lakini kwa sasa yameongezeka.

## 2.7 Mapenzi

Mapenzi ni hali ya kuingiwa moyoni na kumthamini mtu zaidi ya mwingine. Pia huitwa mahaba au nyonda. Imebainika kuwa lengo kuu la kuundwa kwa kikundi cha Maroon commandos lilikuwa ni kuwatumbuiza wanajeshi kambini ili kuwaondolea upweke na ukimwa. Hii ni kwa sababu mara nyingi huwa mbali na familia zao wakitekeleza majukumu yao ya kulinda taifa. Ibainike kuwa wanauhalisia hudhamiria kuisawiri jamii jinsi ilivyo. Suala la mapenzi limejitokeza sana katika nyimbo nyingi za bendi hii. Barbara (Mwimbaji wa bendi ya Maroon), katika mahojiano alieleza kuwa wanajeshi wengi aghalabu huwa na nafasi chache sana ya kujumuika na wanajamii wengi kwa sababu za kikazi na jambo hili huwapa jakamoyo tele. Ili kufidia haya, Maroon Commandos walitoa wimbo "*Kristina dada"* wa kuwafariji na kuwafanya wahisi kuwa wanathaminiwa na wapenzi wao. Ubeti wa kwanza unatoa ufafanuzi zaidi.

*Kristina dada,*

*Uko wapi?*

*Nakutafuta sikuoni,*

*Lakini kwa bahati umenikumbuka,*

*Kwani barua uliyoituma nimeipata,*

*Sasa nakuomba unieleze,*

*Siku ambayo utafika* .(ubeti 1)

Barua inayozungumziwa hapa ni miongoni mwa njia za mawasiliano ya kawaida iliyotumika sana miaka ya themanini. Njia hii inamhakikishia mhusika kuwa anakumbukwa na anathaminiwa na rafiki yake Kristina. Hamu ya kumsubiri umpendaye inawafanya wanajamii kuishi kwa furaha na kuwapa matumaini kwamba wapo wanaowaenzi maishani. Katika jamii ya sasa huu ni wimbo unaowapa wanajeshi matumaini kwa sababu kazi yao ni hatari.

*Siku gani dada,*

*Utakuja,*

*Nikungojee,*

*Sitesheni,*

*Ningekuwa na uwezo,*

*Ningekutumia nauli ya ndege,*

*Ili ufike haraka,*

*Nimekukosa mama,*

*Nimekukosa siku nyingi.* (kiitikio)

Maudhui ya mapenzi yanamashiko katika jamii. Kinyume cha haya ni kukataliwa na binadamu. Anapotengana na ampendaye moyo hujaa simanzi tupu. Wengine huweza kujitia kitanzi na kuuondokea ulimwengu. Katika wimbo *"Usiniambie Unaenda"*, wawili waliopendana wanapotengana huzuni hutawala.

*Sitaki uniambie kuwa unaenda,*

*Haraka unajua haina baraka,*

*Subiri kidogo nikueleze,*

*Usiniache nibaki na wasiwasi,*

*Mpenzi sikia mambo yangu…*

*Naumia sana juu yako mama..*

*Sitaki…sitaki….sitaki….sitaki* (ubeti 1)

Maudhui ya mapenzi yametawala katika nyimbo za Maroon Commandos. Wanajamii wanapojiingiza katika mapenzi ya dhati uhisi kuwa wamethaminiwa zaidi maishani. Hata hivyo, mapenzi haya yanapoingia doa wingu la simanzi hugubika mioyo na haya ni mambo yanayotokea katika jamii na waimbaji hawa wamezungumzia jambo hili kwa kina. Daudi kabaka vilevile amezungumzia suala la mapenzi katika wimbo *"Safari tanganyika"*. Mara nyingi katika jamii ndoa huweza kuvunjika hasa pale ambapo mhusika mmoja anaenda nchi jirani na wote kukaa kipindi kirefu bila kuonana. Hii ni kwa sababu wakati mwingine imani ya watu hupungua na vivyo hivyo kiwango cha mapenzi kwani viwango vya udanganyifu vimeongezeka sana katika ndoa. Hili ni jambo ambalo linahitaji hakikisho la dhati kwa wapendanao. Anasema kuwa:

*Usidhani, nitamwoa mwingine tanganyika,*

*Hata mimi, nikitembea nakuwaza Masita,*

*Nifanyeje, safari yangu sa itavunjika,*

*Nikorendi baby ni shida sheri kwa safari.*

*(nifanye nini baby ni shida ziko kwa safari)* (ubeti 2)

Waimbaji hawa wamefanikiwa pakubwa kudhihirisha kuwa mapenzi katika ndoa ni muhimu sana na endapo udanganyifu hutokea, hamna budi kutalikiana na huo ndio mwanzo wa matatizo katika asasi hii muhimu.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia na kutimiza lengo la kwanza ambalo linahusu maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Maroon Commandos na Daudi Kabaka. Kupitia nyimbo hizi, maudhui ya udaku, ukosefu wa kazi, kutelekezwa kwa watoto, kuombaomba mitaani, uvivu, mafarakano katika ndoa na mapenzi yameshughulikiwa.

Sura inayofuata imeshughulikia lengo la pili la utafiti huu ambalo lahusu matumizi ya tamathali za usemi na jinsi zimechangia katika usawiri wa maudhui katika nyimbo za Maroon Commandos na Daudi Kabaka.

# SURA YA TATU

# MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI KWENYE NYIMBO ZA MAROON COMMANDOS NA DAUDI KABAKA

## 3.0 Utangulizi

Sura iliyopita ilifafanua maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Sura hii imeshughulikia matumizi ya tamathali za semi pamoja na mchango wake katika uwasilishaji wa maudhui katika nyimbo hizi. Hili ndilo lengo la pili la utafiti huu. Inafahamika kwamba tamathali za lugha ni muhimu sana katika kuipa kazi za fasihi uhai. Kulingana na Senkoro (1984), tamathali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii ili kutia nguvu katika maana, mitindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Mwamanda (2008) anasema kwamba tamathali za semi ni viwakilisho au vifananishi vya dhana fulani kwa dhana nyingine zinazofanana. Tamathali hizi hupamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha. Nyimbo zinazochanganuliwa ni miongoni mwa tungo ambazo zimetumia tamathali hizi kwa wingi. Baada ya kuzihakiki nyimbo hizi kwa kina, tamathali zifuatazo zilibainika:

(a) Takriri

(b) Balagha

(c) Tashbihi

(d) Taashira

(e) Chuku

(f) Methali

## 3.1 Takriri

Takriri ni usemi ambao neno au kifungu cha maneno hurudiwarudiwa kwa kusudi la kusisitiza. Mwimbaji huamua kwa maksudi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo kwa lengo maalumu kwa kusisitiza jambo ama kuleta mkazo wa jambo linaloelezwa, (Msokile 1992). Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kwamba takriri huleta mahadhi katika wimbo kwani ule usambamba katika mpangilio wa sentensi huweza kuimbika kwa njia inayopokelewa vizuri zaidi na hadhira. Katika utafiti huu, ilibainika kwamba nyimbo za kikundi cha Maroon Commandos na Daudi Kabaka zimetumia takriri kwa mapana. Odidi, B.(2014) katika makala yaliyochapishwa kwenye gazeti la "Daily Nation"*: In what Direction is Kenyan Music Heading?,* anasema ni kupitia urudiaji huu ambapo hisia kwenye nyimbo hizi zilizopendwa za Kiswahili huwasilishwa kwa njia inayoathiri hadhira lengwa moja kwa moja. Aina mbili kuu za takriri zinajitokeza wazi katika nyimbo zinazorejelewa.

### 3.1.1 Takriri Mishororo

Aina hii ya takriri uhusisha urudiaji wa mshororo au sentensi fulani katika wimbo husika. Kwa mfano, katika wimbo wa *"Pole Musa"* wa Daudi Kabaka, mshororo wa kwanza katika ubeti wa kwanza umerudiwarudiwa. Urudiaji huu si wa kiholela bali umechangia pakubwa katika kuleta mvuto na ridhimu kwenye wimbo huu.

> *Musa nimevumilia sana,*
>
> *Musa nimevumilia sana,* (ubeti 1)

Mishororo hii inaporudiwa hivi huteka makini ya wasikilizaji na imechangia pakubwa katika kukuza maudhui hasa uvumilivu katika ndoa nyingi za kisasa ambazo

zimekumbwa na matatizo mengi. Vilevile katika wimbo *"Tabu ni kwa mwanamume"*, baadhi ya sentensi zimerudiwarudiwa. Kabaka anasema kuwa:

*Ukizaliwa wewe ni kijana,*

*Ukose kazi tabu yote itakupata*

*Ukizaliwa wewe ni kijana*

*Ukose kazi tabu yote itakupata* (ubeti 1)

Mistari hii inasisitiza kuwa suala la kazi ni muhimu katika kukuza uchumi. Mtu yeyote anapokosa kazi shida humwandama. Mishororo hii inawapa changamoto vijana kujishajiisha katika harakati za kujichumia maishani na huu ni uhalisia wa mambo katika jamii.

**3.1.2 Takriri fungu**

Katika wimbo, stanza au kifungu fulani huweza kurudiwa kama korasi au kipikeo. Hii ndio takriri fungu. Kwenye utafiti wetu, ilibainika bayana kuwa mtindo huu umetumika sana katika nyimbo za Daudi Kabaka na Maroon Commandos. Katika wimbo *"viwete"* wa Kabaka, sehemu ifuatayo inarudiwa baada ya kila ubeti kuimbwa.

*Tutasaidia nani mama na mtoto, aeeh mama na mtoto,*

*Tukizaa na kipofu, mtu kizaa na kiwete,*

*Mtu kizaa na bubu chukua mtoto.*

*Aeeh mtoto si mjinga, aeeh mtoto si kipofu*

*Aeeh mtoto si kiwete, aeeh mtoto sio bubu*. (korasi)

Sehemu hii inabainisha ni nani anayehitaji kusaidiwa katika jamii hasa pale mtoto anapozaliwa na mama mlemavu na mwanamume aliyehusika na kitendo hicho kutoroka.

Pia, katika wimbo “Dada Mdaku” wa Maroon Commandos, kifungu kifuatacho kimerudiwa baada ya kila ubeti.

*Wana maroon wameshaona mambo yako si mazuri*

*Tabia zako wewe sio nzuri, bora tukueleze waziwazi.* (korasi)

Mifano hii imethibitisha bayana kuwa takriri imetumika sana katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili na imechangia pakubwa katika kusisitiza ujumbe walionuia waimbaji hawa.

### 3.2 Balagha

Balagha au mubalagha ni maswali ambayo mwimbaji au mhusika hujiuliza bila kutarajia majibu. Lengo la maswali haya ni kuchochea fikra na hisia za hadhira. Katika tasnifu hii, balagha imetumika katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili kutekeleza lengo lilo hilo. Katika wimbo wa Daudi Kabaka “Msichana wa Elimu”, mwimbaji anamwuuliza msichana huyo sababu za kutoolewa ilhali ana maumbile ya kuvutia. Anasema kuwa:

*Msichana wa sura nzuri,*

*Kitu gani kinakufanya usiolewe?* (ubeti 1)

Swali hili linachochea fikra za wasikilizaji kwa sababu msichana mwenyewe ana sifa nyingi zinazotamanika na wanaume wengi wanaohitaji kupata jiko mathalani sura nzuri, elimu ya juu na urembo waa kuvutia kwa jumla. Tatizo lake ni majivuno ambayo ni kizingiti kikubwa katika mahusiano ya kimapenzi. Vilevile katika wimbo “Viwete”, Kabaka anauliza swali linalogusa mioyo ya wasikilizaji la balagha. Anashangaa jinsi ambavyo dada kiwete ambaye hajaolewa huwapata watoto.

*Lakini huyu mtoto amezaliwa na nani?*

*Asiyejiweza ndiye baba wa mtoto*

*Au ni mtu mwenye akili zake?* (ubeti 2)

Maswali haya yanachochea fikra na hisia za wasikilizaji na kuwafanya watafakari kuhusu maisha ya walemavu na mateso wanayopitia mikononi mwa watu wenye akili razini. Katika wimbo wa Maroon Commandos wa "Sofia", wana maroon wametumia maswali ya balagha kuelezea namna ambavyo mhusika Sofia alijifungua watoto na kuwatelekeza. Badala ya kuwatunza aliwatoroka. Wanasema kuwa:

*Watoto uliwazaa, kwa nini uwawache?*

*Rudi nyumbani Sofia eeh, eeh.*

Kitendo chake hakikubaliki katika jamii zetu na swali hili linachochea fikra za wanajamii kuhusu kitendo hiki ambacho kinapigia mfano vitendo vinavyoongezeka katika jamii nyingi kwa sasa. Vilevile, wimbo "Christine Dada", umejaa maswali mengi ya balagha. Wana maroon wanashangaa alikopotelea Kristina ambaye wamemtafuta kila mahali bila kufanikiwa kama ilivyo katika ubeti wa kwanza.

*Kristina dada*

*uko wapi?*

*Nakutafuta sikuoni*. (ubeti 1)

Kwa kila swali linaloulizwa, maswali mengi hutokea akilini mwa wasikilizaji na kuwaathiri kwa namna fulani. Mifano hii ni ishara tosha kuwa mbinu hii imejitokeza katika nyimbo zilizopendwa za Kabaka na Maroon Commandos.

### 3.3 Tashbihi

Tashbihi au mshabaha ni aina mojawapo ya tamathali za semi inayofanya kazi ya kulinganisha vitu viwili visivyo na hadhi sawa kwa kutumia viunganishi kama; mithili ya, mfano wa, sawa na kama vile. Aghalabu aina hii ya tamathali za semi huweza kufanya kazi endapo tu pana vitu viwili vinavyolinganishwa. Mwimbaji Daudi Kabaka katika wimbo "Pole Musa" ametumia tamathali hii anaporejelea kipigo anachokipokea mkewe Musa kila siku mikononi mwa bwana huyu katili.

*Musa nimevumilia sana*

*Musa nimevumilia sana*

*Kupigwa pigwa kama mimi punda,* (ubeti 1)

Punda ni mnyama wa kufuga ambaye hufanyishwa kazi nzito na ngumu. Kwa kawaida yeye huvumilia sana kazi hizi. Mkewe Musa anateswa sana na mumewe kwani anapigwa kila siku na kitendo hiki kinafananishwa na mateso anayoyapitia punda. Katika kibwagizo cha wimbo huu, mkewe Musa anadai kwamba awali alikuwa amenenepa kama "ngoima ya kirike" yaani kama kondoo wa kike. Anasema:

*Kweli Musa, uliponioa,*

*Sura yangu haikuwa na alama hata moja.*

*Nilikuwa na afya nzuri,*

*Nilinona kama ngoima ya kirike.* (korasi)

Vifananishi hivi ni vitu halisi ambavyo hupatikana katika jamii na ambavyo maumbile yake yanafanana. Uvumilivu wa punda na unono wa kondoo unafahamika nahii ni tamathali ambayo imepigia mfano maisha halisi ya binadamu kwani kwa kawaida bibi

anapopitia mateso katika ndoa hukondeana na afya yake kudhoofika. Kinyume chake ni kujinenepea na afya yake kuimarika.

### 3.4 Taashira

Taashira ni kipengele cha tamathali za semi ambapo jina la sehemu ya kitu kimoja au kitu kidogo kinachohusiana na kingine kikubwa hutumiwa kuwakilisha kitu kamili. Kulingana na Senkoro (1982), mwimbaji anapotumia tamathali hii huunda maana mpya kabisa ambayo yahitaji kufasiriwa na hadhira. Katika nyimbo za Daudi na Wanamaroon, taashira imetumiwa lengo lake likiwa ni kuzungumzia swala nzito kwa maneno machache. Katika wimbo "Taabu ni kwa mwanamume" wa Daudi Kabaka, neno kijana limetumiwa kama taashira inayorejelea mwanaume kwa jumla. Mwimbaji anaashiria kuwa yeyote anayezaliwa mwanaume lazima akumbane na changamoto nyingi maishani ikizingatiwa kuwa wana majukumu mengi yakutekeleza maishani. Jamii inamchukulia mwanaume kama kichwa cha familia na ana majukumu mengi ya kutekeleza ili kujikimu yeye na familia yake. Hii ni hali halisi katika tamaduni zetu na moja wapo ya mihimili ya nadharia ya utafiti huu. Kabaka anasema:

> *Ukizaliwa wewe ni kijana,*
>
> *Ukose kazi tabu yote itakupata.*
>
> *Ukizaliwa wewe ni kijana,*
>
> *Ukose kazi tabu yote itakupata.* (ubeti 1)

Pia, katika wimbo "Riziki" wa wanamaroon, neno hili ni taashira ya jinsi binadamu anavyofaa kutia bidii ili ayapate mafanikio maishani. wanasema kuwa:

*Kazana…kazana mwana,*

*Pengine utafanikiwa.*

*Riziki riziki mwana,*

*Haivutwi kwa kamba.* (ubeti 3)

Waimbaji hawa wanapotumia tamathali hii, wana maana tofauti na maana ya moja kwa moja ya neno kijana na riziki.

**3.5 Chuku**

Chuku ni mbinu ya kutumia maneno yaliyotiliwa chumvi ili kusisitiza ujumbe fulani au kusifia kitu. Lengo kuu ni kufanya kinachosimuliwa kivutie zaidi. Mbinu hii ni muhimu sana katika kupamba lugha kwani kazi husika hupendeza zaidi kwa kutiliwa chumvi na hasa maneno ya uwongo yanapoongezewa. Kwenye utafiti huu, ilibainika kwamba chuku ni mbinu ambayo imetumika sana katika nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na Maroon Commandos. Kwa mfano, katika wimbo "Taabu ni kwa mwanaume" wa Daudi Kabaka, ni chuku kwa mwimbaji kudai kwamba endapo mtoto atazaliwa kijana (yaani mvulana kulingana na muktadha wa mtunzi), atakumbwa na taabu zote duniani. Anasema kuwa:

*Ukizaliwa wewe ni kijana, ukose kazi taabu yote itakupata.*

*Ukizaliwa wewe ni kijana, ukose kazi taabu yote itakupata*. (ubeti 1)

Kipindi kinachozungumziwa hapa ni enzi za ukoloni na baada ya ukoloni nchini Kenya. Katika wakati huu, mtu aliyechukuliwa kuwa na kazi sanasana ni yule ambaye aliajiriwa mijini ama kwenye mashamba makubwa ya matajiri vijijini. Pia, katika kipindi hiki, kuajiriwa kwa mtoto wa kike hakukuthaminiwa sana katika utamaduni wa kiafrika.

Kwa sasa hayo si kweli kwani kazi zipo ama za kuajiriwa au kujiajiri mashambani na mijini kwa jinsia zote kwa hivyo swala hili limetiliwa chumvi.

Wana maroon nao katika wimbo wao “Kristina dada” wanaongezea chuku kwa kuimba:

*Siku gani dada, utakuja,*

*Nikungojee stesheni.*

*Ningekuwa na uwezo,*

*Ningekutumia nauli ya ndege.*

*Ili ufike haraka.*

*Nimekukosa siku nyingi,*

Maneno kama haya hutumiwa sana katika nyimbo za mapenzi. Aghalabu huwa ni chuku kwa sababu chuku husheheni maneno mengi matamu ambayo ni uwongo. Waimbaji hawa wawili wamefanikisha tamathali hii.

**3.6 Methali**

Methali ni tungo fupi za kisanaa ambazo hutoa wosia au nasaha kwa lugha ya kimafumbo. Kulingana na Maitaria (2012), methali kama kaulu za makusudi hutegemea athari itakayoibushwa katika hadhira. Anasema kwamba mtunzi hajitungii yeye mwenyewe ila hutunga kwa mathumuni ya kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Haya yanamaana kuwa lazima awe mwenye hadhari kubwa katika uteuzi wa kauli au msamiati uliotumika ili kazi isimkinaishe msomaji kwa hivyo lazima atumie lugha teule. Katika nyimbo vivyo hivyo, lazima mtunzi atilie maanani kiwango cha ufahamu, mielekeo na hisi za

wasikilizaji au wapokezi. Katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za Daudi Kabaka na Maroon Commandos, methali zimetumika ili kutilia nguvu ujumbe unaopitishwa kimafumbo. Wimbo “Usiniambie unaenda” wa Maroon Commandos umetumia methali katika ubeti wa kwanza. Wanasema kuwa:

*Sitaki uniambie kuwa unaenda,*

*Haraka unajua haina Baraka,* (ubeti wa 1)

Msitari wa pili ni methali inayosema kuwa “*Haraka haraka haina baraka*.” Waimbaji hawa wanamshauri dada anayerejelewa kwamba ni muhimu kuwa na subira na kumpa mpenzi wake muda ili wajadiliane kuhusu uhusiano wao kwani si vyema kila mara wanapokutana kusema ana haraka au ana jambo la dharura ambalo anahitaji kulishughulikia. Vilevile katika wimbo “Riziki”, methali zifuatazo zimetumika katika ubeti wa kwanza na wa tatu mtawalia.

*Haba na haba hujaza kibaba.*

*Riziki haivutwi kwa kamba*. (ubeti wa 1 na 3)

Methali ya kwanza inamshauri mhusika anayerejelewa kwamba yafaa ayapangie mapato yake madogo na mwishowe atakuwa na kipato kikubwa. Methali ya pili pia inamshauri ajitume maishani katika kusaka mali kwani mafanikio ama riziki hupatikana baada ya mchakato fulani kutekelezwa. Mifano hii ni ithibati kwamba nyimbo hizi zimepambwa vizuri kwa matumizi ya mafumbo haya.

### 3.7 Hitimisho

Sura hii imefanikiwa kushughulikia lengo la pili la utafiti ambalo linahusu matumizi ya tamathali za semi pamoja na mchango wake katika ujenzi wa maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Imehakikiwa kwamba nyimbo hizi zimetumia takriri, balagha, tashbihi, taashira, chuku na methali kwa wingi. Sura inayofuata nayo imeshughulikia lengo la tatu la utafiti ambalo linahusu kufafanua ulinganifu uliopo katika nyimbo za Daudi Kabaka na kundi la Maroon Commandos.

# SURA YA NNE

# ULINGANIFU KATI YA NYIMBO ZA DAUDI KABAKA NA MAROON COMMANDOS

## 4.0 Utangulizi

Sura iliyopita iliangazia matumizi ya tamathali za semi katika uwasilishaji wa maudhui katika nyimbo za Maroon Commandos na Daudi Kabaka. Sura ya nne imeshughulikia lengo la tatu la utafiti huu. Lengo hili linaangazia ulinganifu uliopo kati ya nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Fasihi ni utumiaji wa lugha kisanaa. Vipengele vya kifasihi vinaweza kulinganishwa na kulinganuliwa na vipengele vingine vya fasihi pia. Kulingana na Keesey (1998), njia ya kusoma inaweza kuwa taaluma ya kusoma vilevile. Anaeleza kuwa somo linaweza kutii masharti ya kisayanzi kwa kujikita katika majaribio na kutoa maamuzi maalumu yanayotokana na majaribio hayo. Maoni haya yameelekeza lengo la sura hii. Nyimbo zilizotungwa na vikundi hivi zinashabihiana kwa kiwango kikubwa. Mihimili ya nadharia ya uhalisia imetumika katika kuchanganua lengo hili. Hii ni kwa sababu dhima kuu ya mtunzi ni kuionyesha jamii jinsi ilivyo. Watunzi hawa waliishi katika kipindi kimoja cha kihistoria ijapokuwa wote walikuwa na njia tofauti za kujipatia pato au kuchuma. Kwake msanii Daudi Kabaka, muziki ulikuwa ni njia ya kujipatia riziki maishani ilhali wana Maroon walichukulia muziki kama shughuli ya ziada baada ya kukamilisha majukumu yao ya kila siku ya kijeshi na kuimba waliweza kukupenda mno. Baada ya ukusanyaji na uhakiki wa nyimbo hizi kwa kina, vigezo vifuatavyo vilitumika katika uchambuzi ili kubainisha ulinganifu unaojitokeza katika nyimbo zinazorejelewa:

(a) Mazingira

(b) Utamaduni

(c)Mwingiliano wa maudhui

(d) Uteuzi wa lugha

(e) Mtindo wa usimulizi

(f) Usawiri wa wahusika

**4.1 Mazingira**

Mazingira ya msanii ni muhimu sana katika kuelewa kazi yake. Nyimbo kama tungo za sanaa aghalabu huongozwa na mtazamo wa mwimbaji kuhusu maisha yake na yale yanayomzunguka. Mtazamo huu huongozwa na mwelekeo wake kuhusu maisha, muono wake na hata itikadi kwa sababu nyimbo hutungwa kutokana na hisi za mtu. Dhamira ya wimbo hujikita katika mambo ambayo mwimbaji huyaona, huyasikia na hata kuyashuhudia. Daudi Kabaka aliishi jijini Nairobi. Kutokana na kushuhudia maisha ya mjini, baadhi ya nyimbo zake zilihusu jinsi wanajamii hukumbana na changamoto za mijini. Nyimbo zake maarufu kama vile *Shauri moyo twist* na *viwete* zinadhihirisha jinsi watu hupitia masaibu mengi mjini kutokana na ujanja na ulaghai wa wenyeji. Anakutana na mwanamke ambaye anamdanganya kuwa yeye katu hajaolewa kwa sababu ana mipango ya kibinafsi. Udanganyifu huu unamshawishi mhusika kwenda mpaka kwa mwanadada huyu katika mtaa wa Shauri moyo jijini Nairobi kwenye chumba cha mwanamume mwingine. Anasema kuwa:

*Nilikuta bibi wa kwanza Nairobi,*

*Akanipenda na mimi nikampenda.*

*Nikamwuliza kama ana bwana,*

*Akanijibu sina hata mpenzi.* (ubeti 1)

Licha ya kwamba nyimbo hizi ni za ubunifu, maswala ya wanawake kuwadanganya wanaume kwamba hawana mabwana ili wajinufaishe yameenea sana mijini. Tabia kama hizi zimeenea sana hasa mijini na hata ni miongoni mwa njama ambazo zinatumiwa na watekaji nyara kuwaibia watu pesa kwa kudai fidia ili mateka waachiliwe. Hili ni jambo halisi katika jamii. Kikundi cha wana Maroon pia kilibuniwa jijini Nairobi. Habel Kifoto na wenzake walinuia kutumbuiza wanajeshi wenzao kambini. Licha ya kwamba mazingira yao ni ya jeshini, wamejaribu sana kuonyesha uhai na kujileta karibu na wanajamii ambao ndio hadhira halisi. Wamefanya hivyo kupitia nyimbo zao ambazo zinazungumzia kuhusu maisha ambayo wanakabiliana nayo wanajamii kila siku. Nyimbo zao kama vile *Ewe Sofia* na *Dawa nimuone hani* hugusa mtima unapozisikiliza. Nyimbo hizi zinaonyesha kwamba licha ya kuwa wao hufanya kazi ya kulinda nchi, wana majukumu mengine ya kushughulikia familia na kama binadamu yeyote wana hisia. Nyimbo hizi zinawafanya wajinasibishe na zile changamoto nyingi ambazo humkumba mwanadamu maishani. Wanasema:

*Ewe sofia,*

*Mimi niko kwetu.*

*Hapa sina shida,*

*Hata watoto pia hawana neon.*

*Wewe uliniacha,*

*Ukaenda kwenu.*

*Yote yalinipata,*

*Nikavumilia* (ubeti 1,2)

Waimbaji hawa walikulia katika mazingira sawa ya mijini. Kulingana na Oluoch Kanindo aliyekuwa mtayarishi wa nyimbo, kufanikiwa kwao miaka ya sabini kulitokana na kuwepo kwa mashirika mawili makuu ya pekee yaliyokuwa yakirekodi nyimbo ya E.M.I na C.B.S jijini Nairobi. Kwa hivyo, mazingira haya, maisha ya mjini na vifaa vya kurekodi vilichangia pakubwa katika kufanikisha maudhui na kupanua hadhira pokezi.

## 4.2 Utamaduni

Utamaduni ni mila, asili na desturi za kundi la jamii fulani. Kulingana na kamusi ya TUKI (2004), utamaduni huhusisha yale mambo changamano kuhusu maarifa, imani, sanaa, maadili, desturi au mila katika jamii. Utamaduni wa watu hutambuliwa kupitia jinsi watu wanavyoishi, elimu yao na falsafa zao. Wanauhalisia husawiri jamii jinsi ilivyo bila kupigia chuku jambo lolote. Waimbaji hutilia maanani utamaduni wa hadhira lengwa ambayo ndio wapokezi wa nyimbo zao. Baada ya kuhakiki nyimbo za Daudi Kabaka na Maroon Commandos, wote wamezungumzia mila na desturi za wanajamii hasa tamaduni kuhusu ndoa na malezi. Utafiti huu umebainisha kuwa waimbaji hawa wamezungumzia jinsi ambavyo ndoa ni muhimu katika jamii. Kipengele kingine cha utamaduni ambacho

kimeangaziwa ni suala la ndoa. Wimbo "*Msichana wa Elimu"* unaonyesha kuwa kiwango cha juu cha elimu cha mtu yeyote kisiwe kikwazo cha kuondokewa na fikra kuhusu umuhimu wa kupata jiko. Jamii huendelezwa kupitia ndoa na hii ndio sababu kikundi cha Daudi Kabaka kinamkashifu msichana ambaye hataki ndoa. Wanajamii wanamchukulia mtu kama huyu mwasi wa mila na tamaduni za jamii husika na hivyo kuwa mtumwa miongoni mwa wanajamii wenyewe. Wanasema kwamba yeyote anayekaidi ndoa ama kwa kuchelewa kuolewa au kusababisha kusambaratika kwa ndoa hizi anakashifiwa na jamii iyo hiyo. Wimbo "*Msichana wa elimu"* wa Daudi Kabaka umethibitisha haya.

*Msichana wa urembo kama wewe,*
*Huonyeshe mapenzi kwa vijana,*
*Ukionyesha majivuno kwa vijana,*
*Utazeeka ukiwa kwenu* (ubeti 3)

Vilevile, nyimbo *"Dada Mdaku"* na "*Christina Dada"* za wana Maroon ZImefanikiwa kuonyesha kuwa ndoa lazima itunzwe la sivyo itasambaratika.

Utamaduni mwingine ambao umetiliwa maanani na waimbaji hawa ni malezi. Suala la kuwalea watoto ili wawe watu waadilifu katika jamii limezungumziwa na wote. Maroon Commandos kupitia wimbo *"Sofia"* wanasisitiza haja ya kuwalea watoto unapowazaa bila kuwatelekeza. Mlezi wa kwanza wa mtoto ni mama na endapo atakosa huduma zake kwa sababu ya kutoroka kwake, jambo hili humwathiri kisaikolojia. Wanasema:

*Rudi kaone watoto,*

*Rudi nyumbani Sofia aeeh,*

*Rudi kaone watoto ooh* (ubeti 2)

Wimbo mwingine "*Ewe Sofia"* unaonyesha jinsi mwanaume hutaabika hasa mke anapomwacha ama kwa kutoroka au kutalikiwa. Inamlazimu amtafute mke mwingine kwani jukumu la kuwalea watoto huwa rahisi pale wanaposaidiana wazazi wakiwa wawili. Anaeleza kuwa:

*Mimi nakujulisha,*

*Ukae ukijua,*

*Kwamba hapa nilipo,*

*Nilimwoa mwingine hivi majuzi.* (Ubeti 2)

Daudi Kabaka pia, anashauri jamii nzima kuambaa uvivu ili kufanikisha maisha ya kila mwanajamii kupitia wimbo "*Uvivu adui ya maendeleo"*. Hii ni kwa sababu kila jamii iliweka mikakati ya kuwafunza wanao namna ya kutekeleza majukumu yanayowalenga wangali wadogo kupitia mafunzo ya jandoni na unyagoni. Mtu ambaye hapendi kufanya kazi anachukuliwa kama ambaye hana faida yoyote katika ujenzi wa taifa.

Ulezi kwa hivyo ni swala halisi katika jamii na lazima kila mtu alitilie maanani la sivyo jamii nzima itaporomoka. Kupitia nyimbo hizi, utamaduni ni muhimu kudumishwa kwani mwacha mila ni mtumwa. Vilevile, imebainishwa kuwa yeyote anayeenda kinyume na mila na tamaduni za jamii huathirika kwa namna fulani.

Tamaduni zote pia zinasisitiza umuhimu wa kudumisha maadili katika jamii. Mambo au vitendo ambavyo vinakiuka maadili hukashifiwa. Wimbo "Masita" wa kikundi cha Daudi

Kabaka unasisitiza umuhimu wa kudumisha mapenzi ya dhati kwa kutomwendea mke kinyume kwa kutafuta changu ndoa hasa pale ambapo wana ndoa wanaishi maeneo mbalimbali ama kwa kazi au safari. Wanasema:

*Usidhani, nitamwoa mwingine Tanganyika,*

*Hata mimi, nikitembea nakuwaza masita,*

*Nifanyeje, safari yangu sa itavunjika,*

*Nikorendi baby ni shida sheri kwa safari,*

*Nikorendi baby ni shida sheri kwa safari {Nifanye nini baby ni shida ziko kwa safari}* (ubeti2)

Mifano hii inaonyesha kwamba vikundi hivi viwili vimetunga nyimbo nzuri ambazo zimeetilia maanani utamaduni ambao ndio nguzo au msingi wa kujenga na kuongoza jamii.

**4.3 Mwingiliano wa Maudhui**

Maana ya kazi za fasihi hutegemea miundo, kanuni na utamaduni zinakopatikana. Kazi hizi zinaweza kuwa zilitungwa katika kipindi kimoja na kuwa na uhusiano wa kimaudhui. Nyimbo zilizopendwa za Daudi Kabaka na Maroon Commandos ziliimbwa katika kipindi kinachokaribiana na vilevile, makundi haya mawili yaliweza kuimba pamoja mwaka wa elfu mbili na nane waliposhirikiana katika kutoa wimbo "*Kenya unite"* wakati wa vita vya baada ya uchaguzi nchini Kenya mwaka wa 2007-2008. Kwa vikundi hivi, maudhui mengi yanayozungumziwa katika sura ya pili yanajitokeza katika nyimbo zao. Hii ni kwa sababu filosofia yao kuhusu maisha inaongozwa na imani kuwa maisha ya binadamu na utangamano ni muhimu kwani wana jamii lazima waishi pamoja. Maudhui haya

yanaweza kugawanywa katika makundi mawili: Maudhui ya kijumla ambayo yamekuwepo katika jamii na maudhui ibuka. Maudhui ya kijumla ni kama vile: udaku, kutelekeza watoto, uvivu, mafarakano katika ndoa na mapenzi. Udaku umeelezwa kama tabia ya kuchungua na kutaka kujua mambo ya watu yaani umbeya. Kutelekeza watoto kumefafanuliwa kama tabia ya kutowapa watoto mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi, makazi na elimu nzuri. Uvivu ni uzembe ama tabia ya kutotaka kufanya kazi. Mhusika huwa amelegea katika jambo analolifanya na kuabudu ulofa. Mafarakano katika ndoa ni kule kutoelewana kati ya wanandoa. Ukosefu wa kazi na ombaomba mitaani kumechangiwa pakubwa na watu kuhamia mijini kutafuta kazi za ofisi. Wengi wameacha kazi za shambani na kuhamia mijini na kazi wanazopania kuzipata zinakosekana. Wanajamii hawa wanapozikosa kazi hizi, hubuni mbinu za kujipatia riziki zikiwemo utapeli kwa njia ya kuombaomba mitaani. Haya yamethibitishwa katika wimbo *"viwete"*.

*Wanaume maskini huomba njiani,*
*Saidia maskini akishalewa pombe.*
*Mtu mwenye shida,*
*Akipata kidogo, hutumia kwa shida zake,*
*sio kulewa pombe*. (ubeti 3)

Maudhui mengine ibuka ni kama vile vita vya kikabila. Maudhui ya ndoa na mapenzi pamoja na mafarakano kwenye ndoa hizo yametiliwa maanani kwani haya ni mambo halisi yanayotokea katika jamii na kuiathiri moja kwa moja mambo ambayo ndicho kiini cha utafiti huu. Kupitia nyimbo "*Msichana wa elimu, Dada mdaku na Kristina dada",* asasi ya ndoa imetiliwa maanani kwani ndoa yaweza kutofanikiwa endapo kuna wale wanaoihujumu kama alivyofanya "Dada mdaku".

### 4.4 Uteuzi wa Lugha

Uteuzi wa lugha itakayotumiwa katika utunzi wa nyimbo katika fasihi huwa na umuhimu mkubwa hasa katika uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira. Ili kazi ya fasihi ifikie hadhira pana, lugha rasmi ama ya taifa huwa inafaa zaidi kutumiwa. Kulingana na Ngugi (2000), sababu kuu iliyofanya nyimbo zilizopendwa za Kiswahili kuwa maarufu ni matumizi yake ya lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu lugha hii huwa inawafikia watu wengi wa Afrika mashariki na inafananishwa na lingua franka ya eneo hili. Jacobson (1960), anazungumzia matumizi ya lugha ya fasihi katika viwango viwili yaani metonimia na istiari. Anasema kwamba lugha inayopendwa zaidi ni ile iliyosheheni mafumbo na maudhui yake ni yale ya moja kwa moja. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya na haina ukabila na ndiyo inayotumiwa mashambani na mijini katika hafla mbalimbali. Nyimbo zinazorejelewa katika utafiti huu za vikundi vya Daudi Kabaka na wana Maroon zilijipatia umaarufu kwa wakenya kwa sababu ya kuimbwa kwa lugha ya Kiswahili. Japo zipo nyimbo zao ambazo ziliimbwa kwa lugha zao asilia kama vile "*Charonyi ni wazi*", nyimbo zinazorejelewa katika utafiti huu ni zile walizoziimba kwa Kiswahili na wote wamelingana kwa kuteua lugha hiyo. Kabaka ametumia maneno na vifungu vya lugha zingine mbali na Kiswahili na ambazo zimetafsiriwa ili kufanikisha utafiti huu. Wimbo "*Safari ya tanganyika"* umetumia baadhi ya maneno ya kiluyha.

*Usidhani, nitamwoa mwingine Tanganyika*

*Hata mimi, nikitembea nakuwaza Masita*

*Nifanyeje, safari yangu sa itavunjika*

*Nikorendi baby ni shida sheri kwa safari* {Nifanye nini baby ni shida ziko kwa safari}

*Nikorendi baby ni shida sheri kwa safari* {Nifanye nini baby ni shida ziko kwa safari} (ubeti 2)

Pia, katika wimbo "*Pole Musa"* maneno "*Ngoima ya kirike"* ambayo ni lugha ya Kikikuyu yametumiwa kumaanisha kondoo wa kike. Lugha hizi za kimaeneo hufikia hadhira finyu sana hasa katika uwasilishaji wa ujumbe japo mdundo na mahadhi yake yanaweza kupendwa na hadhira ya jamii pana.

Waimbaji hawa pia wameshabihiana katika uteuzi wa lugha yenye tasfida na tamathali zingine za lugha katika kuzirembesha nyimbo zao. Nyimbo zao zilizingatia matumizi ya lugha yenye adabu hata pale masuala mazito kama vile ukahaba na ngono yanapozungumziwa. Daudi Kabaka katika nyimbo zake "*Bibi wa Nairobi* na *Viwete"* zimedhihirisha hayo.

*Tukaenda naye mpaka kwake,*

*Shauri moyo kwa nyumba za tumbako.*

*Nilipolala kasikia hodihodi,*

*Fungueni ni mimi mwenye nyumba.* (ubeti 2)

Kwa upande wa wana Maroon, wimbo *"Ewe Sofia*" uliimbwa katika hali ya masikitiko. Mwimbaji ijapokuwa amekasirishwa na kutoroka kwa mkewe na kuachiwa watoto, hatoi maneno makali yenye matusi kwake. Anajipa moyo kwa yote yanayoendelea tangu watengane.

*Mimi nakujulisha,*

*Ukae ukijua ,*

*Kwamba hapa nilipo,*

*Nilimwoa mwingine hivi majuzi.* (ubeti 2)

Waimbaji hawa pia walifanikiwa pakubwa katika kutumia methali ambazo ni mafumbo yanayopigia mfano maisha halisi ya mwanadamu. Methali kama vile *riziki haivutwi kwa kamba, haba na haba hujaza kibaba na haraka haraka haina baraka,* ni muhimu sana katika kushauri vizazi vya sasa na vya baadaye. Jamii inashauriwa kutia bidii ili kujipatia riziki ambayo haipatikani bila kutia juhudi. Pia, wanajamii wanashauriwa kuhifadhi kile wanachokipata kidogokidogo kwa matumizi ya baadaye kwani ubadhirifu una hasara zake. Vijana nao wanashauriwa kutokuwa na pupa katika harakati zao za kusaka mali katika methali *haraka haraka haina baraka*. Mifano hii imebainisha kwamba waimbaji hawa wamelingana katika uteuzi wa lugha maalumu katika nyimbo zao hasa lugha ya taifa na vilevile lugha safi iliyosheheni mafunzo yanayopitishwa kwa njia ya adabu na heshima.

## 4.5 Mtindo wa Usimulizi

Mtindo ni jinsi msanii anavyotumia ufundi, umahiri na hisia zake katika kutenda au kuelezea jambo fulani. Kulingana na Senkoro (1982), mtindo ni jumla ya mbinu zinazomwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe. Kwa hivyo, mtindo ni ule upekee alionao mtunzi wa kazi ya fasihi kuwasilisha kazi yake. Ijapokuwa uwasilishaji huu unahusu vipengele vingi kama vile uteuzi wa wahusika, hisia za mwandishi, namna anavyopanga sura, mandhari, semi na vinginevyo, namna ya usimuliaji ndiyo imetiliwa maanani katika utafiti huu. Usimulizi ni namna msanii anavyotumia kauli mbalimbali za usimuliaji katika kueleza visa na matukio kwa vile alivyopangilia katika bunilizi zake. Katika usimuliaji huu, waimbaji hawa wametumia mbinu tofauti kama vile hadithi, visa na mikasa, matukio ya kihistoria, tajriba za kibinafsi na nyinginezo. Nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za vikundi vya Daudi Kabaka na Maroon Commandos zimewasilishwa kwa mtindo wa

kusimulia visa kama ilivyo katika hadithi. Nyimbo zilizoteuliwa katika utafiti huu japo ni bunilizi zimetolewa kama visa au hadithi za kweli zinazotokea katika jamii halisi. Hadithi hizi zina mtiririko ambao hadhira huweza kuzifuatilia kuanzia mwanzo hadi mwisho na ujumbe humfikia msikilizaji kwa njia inayoeleweka zaidi. Wimbo wa Kabaka "*Bibi wa Nairobi"* wa unasimulia kuwa:

*Nilikuta bibi wa kwanza Nairobi,*
*Akanipenda na mimi nikampenda,*
*Nikamwuliza kama ana bwana,*
*Akanijibu sina hata mpenzi.* (ubeti 1)

Usimulizi wa kisa chenyewe unaishia pale anapogundua kuwa mhusika huyu ameolewa. Hiki ni kitendo ambacho kingefanya wapigane na kuumizana. Visa kama hivi hutokea katika jamii ambayo maadili yamedorora na athari zake huwa mbaya. Wimbo "*pole musa"* ni kisa na mkasa unaosimuliwa kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mkewe Musa aliolewa akiwa na afya nzuri. Baadaye dume hili linageuka na kuwa bahili. Kutokana na ulevi, linaanza kumpiga mkewe kitendo ambacho kinamfanya aombe talaka kwani mateso hayo yalikuwa yamepita mipaka. Katika jamii halia, wanaume wengi wamekuwa wakiwapiga wake zao kwa sababu ya ulevi. Katika jamii ambayo imebadilika, wanaume nao hutiwa mikononi na wake zao wanaporejea kutoka ulevini. Mambo haya yamesababisha kutengana kwa familia husika.

Maroon Commandos katika wimbo "*Kristina dada"* anaanza kisa kwa kuuliza swali linalomdokezea msikilizaji kuhusu kisa kizima. Anaanza kwa kusema kuwa:

*Kristina dada,*

*Uko wapi?*

*Nakutafuta sikuoni,*

*Lakini kwa bahati umenikumbuka,*

*Kwani barua uliyoituma nimeipata…* (ubeti 1)

Mdokezo huu unaashiria kwamba mhusika Kristina hajaonekana kwa siku nyingi ama kwa kuondoka kwa hiari au kutoroka na kumwachia mwenzake jakamoyo na hali hii imemsukuma amtafute kwa udi na uvumba.

Katika uhitimishaji wa kisa chenyewe, mwimbaji anatarajia kuwa huenda wakutane japo hajui siku yenyewe. Anabaki akitumainia ipo siku ambayo watakutana ingawa hajui ni wakati upi wa kurejea kwa Kristina. Anasema kuwa:

*Siku gani dada?*

*Utakuja.*

*Nikungojee,*

*Sitesheni.*

*Ningekuwa na uwezo,*

*Ningekutumia nauli ya ndege.*

*Ili ufike haraka.*

*Nimekukosa , mama*

*Nimekukosa siku nyingi.* (ubeti 3)

Katika wimbo mwingine *"Ewe Sofia"*, Maroon Commandos wanasimulia kuhusu namna mhusika alivyotalikiana na mkewe hadi akafikia kiwango cha kumwoa mke mwingine ili achangie katika malezi ya watoto wake. Anasema:

*Wewe uliniacha,*

*Ukaenda kwenu.*

*Yote yalinipata,*

*Nikavumilia.*

*Mimi nakujulisha,*

*Ukae ukijua.*

*Kwamba hapa nilipo,*

*Nilimwoa mwingine hivi majuzi.* (Ubeti 3,4)

Katika mtindo pia, nyimbo nyingi zilizoimbwa na kikundi kilichoongozwa na Daudi Kabaka ni fupifupi. Sentensi zake na beti ni fupi pia. Huwa tatu ama nne pamoja na kipokeo chake. Nyimbo "*Shauri moyo twist, Pole Musa, Safari ya tanganyika, taabu kwa mwanamume, msichana wa elimu, Kabaka says,* na *vijana wa mjini"* zilizotumika sana katika kazi hii zinadhibitisha haya. Nyimbo za kikundi cha wana Maroon ni ndefu sana. Urefu huu umechangiwa pakubwa na urudiaji mwingi wa beti na kipokeo katika uimbaji wa nyimbo zenyewe. Nyimbo *"Ewe Sofia, Kristina dada, amka kumekucha, dawa nimuone hani, usiniambie unaenda, riziki* na *dada mdaku'* ni ndefu mno na kwa hivyo basi, zimeweza kutofautiana kwa kuzingatia kigezo cha urefu.

Mifano iliyotolewa ni ithibati kuwa nyimbo zilizoteuliwa katika utafiti huu zimewasilishwa kama hadithi zilizosimuliwa ila zimepangwa katika beti na mtindo huu unadhihirisha kuwa kuna ulinganifu katika nyimbo za waimbaji hawa tofauti na baadhi ya wasanii wa kizazi kipya ambao nyimbo zao hutawaliwa na midundo ya kipekee kama vile kufokafoka na ujumbe haujitokezi moja kwa moja.

**4.6 Usawiri wa Wahusika**

Wahusika ni wale washiriki ama waliotajwa katika kazi yoyote ya fasihi. Wanaweza kuwa watu, wanyama, ndege, majini na hata viumbe wengine wasioishi. Viumbe hawa hubuniwa na mwandishi ili kufanikisha uwasilishaji wa kazi yake. Mambo yatendwayo na wahusika wa kazi ya fasihi ni yale ya kawaida katika maisha yetu. Nyimbo zilizopendwa za Kiswahili kama tungo zingine za fasihi simulizi zimetumia wahusika halisi katika uwasilishaji wa maudhui yao. Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida wanaopatikana katika jamii halisi, kuyachunguza na kusimulia maisha yao, tajiriba zao na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Daudi Kabaka na Maroon Commandos wamewateua wahusika katika nyimbo zao na kuwapa majina yanayopatikana katika jamii tunamoishi. Wahusika hawa ndio wanaotumika katika kujenga maudhui kupitia masimulizi yanayopatikana katika nyimbo zao. Katika wimbo *"Kristina dada"*, wa Maroon Commandos, Christine ni jina la kike linalotumiwa sana na jamii ya wakristo. Huyu ni mhusika halisi anayetumiwa katika wimbo kusimulia jinsi alivyotoweka asijulikane aliko lakini anawasiliana na mwimbaji kupitia kwa barua.

> *Kristina dada,*
>
> *Uko wapi?*
>
> *Nakutafuta sikuoni*
>
> *Lakini kwa bahati umenikumbuka*
>
> *Kwani barua uliyoituma nimeipata….*(ubeti 1)

Mhusika Sofia vilevile ametumika katika nyimbo mbili tofauti za "*Ewe Sofia* na *Sofia"* mtawalia. Katika nyimbo hizi, Sofia ni mwanamke aliyeishi katika ndoa kwa muda fulani na kujifungua watoto kadha. Baadaye anawaacha na kujiendea kusikojulikana na

kuwaacha na mumewe kuwalea. Katika wimbo wa pili “*Sofia”*, baba watoto amelazimika kumwoa mke mwingine amsaidie katika malezi ya watoto wake.

Daudi Kabaka ameteua mhusika *Msichana* ambaye amepewa sifa kama vile mwenye elimu nzuri na sura ya kupendeza katika kubainisha jinsi wanawake wenye sifa kama hizi hawataki kuolewa. Katika wimbo “*Pole Musa”*, Musa ni kielelezo cha wanaume ambao hulewa na kuvuruga mabibi zao hasa kwa kuwapiga. Kitendo hiki huwafanya wadhoofike kiafya na hatima yao ni kutoroka ndoa za aina hii. Waimbaji hawa wameteua wahusika wanaopatikana katika jamii halisi katika nyimbo zilizoteuliwa katika utafiti huu. Matendo wanayotekeleza pia yanafanyika katika jamii kwa hivyo vikundi hivi vimeshabihiana kwa namna walivyoteua wahusika wao.

**4.7 Hitimisho**

Sura hii ya nne imebainisha na kutimiza lengo la tatu la utafiti huu ambalo linahusu ulinganifu uliopo kati ya nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za vikundi vya Daudi Kabaka na Maroon Commandos. Haya yamefanikishwa kupitia mtazamo wa vipengele kama vile mazingira, utamaduni, mwingiliano wa maudhui, u teuzi wa lugha, mtindo wa usimulizi na usawiri wa wahusika.

Sura inayofuata ya tano imeshughulikia muhtasari wa utafiti huu, hitimisho na vilevile mapendekezo ya tafiti zingine za baadaye zenye uhusiano na utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa sura zilizojadiliwa katika tasnifu hii. Pia, matokeo ya utafiti yaliyoongozwa na malengo ya utafiti pamoja na yaliyoandikwa kuhusu nyimbo zilizopendwa za Kiswahili na kuhifadhiwa kwenye santuri na vifaa vingine vya kielektroniki yameshughulikiwa. Sura hii vilevile, imeweza kutoa mapendekezo yanayonuia kufaidi wasomi na watafiti wa tafiti za baadaye.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Tasnifu hii ilinuia kubainisha maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili kwa kulinganisha msanii Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Pia, matumizi ya tamathali za usemi katika uwasilishaji wa maudhui katika nyimbo zilizoteuliwa yaliweza kuangaziwa. Tasnifu hii vilevile, ilidhamiria kubainisha ulinganifu uliopo kati ya nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza imezungumzia kuhusu Usuli wa mada ya utafiti yaani *"Maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili: Mtazamo linganishi wa Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos"*. Suala la utafiti limeshughulikiwa. Katika sura hii, maswali ya utafiti pamoja na malengo mahususi yaliyoongoza utafiti wenyewe yameorodheshwa na kuangaziwa kwa kina. Sababu kuu za kuchagua mada zimefafanuliwa kwa tuo. Sababu kuu ni maudhui yanayowasilishwa na nyimbo zenyewe. Aidha, nyimbo hizi zinatumika sana kwa sasa katika vyombo

mbalimbali vya mawasiliano. Upeo na mipaka ya utafiti imebainishwa katika sura hii pamoja na yaliyoandikwa kuhusu mada yenyewe. Sura hii imehakiki nadharia ya uhalisia iliyotumika katika utafiti huu, mbinu za utafiti, mahali pa utafiti, sampuli lengwa, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data yote umechanganuliwa katika sura hii ya kwanza.

Sura ya pili imechanganua maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za msanii Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Maudhui yaliyochanganuliwa ni yale yanayoambatana na maisha halisi yanayomkumba mwanadamu katika maisha ya kila siku. Maudhui hayo yanaoana na nadharia teule ya uhalisia iliyoongoza utafiti huu. Maudhui hayo ni pamoja na: udaku, ukosefu wa kazi, kutelekezwa kwa watoto, ombaomba mitaani, uvivu, mafarakano katika ndoa na mapenzi. Ufafanuzi wa maudhui haya uliweza kufanikisha utafiti wa tasnifu hii.

Sura ya tatu imeshughulikia matumizi ya tamathali za usemi pamoja na mchango wake katika uwasilishaji wa maudhui kwenye nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Tamathali ambazo zimechanganuliwa zilijitokeza sana katika nyimbo zilizoteuliwa katika utafiti huu. Mbinu ambazo zilijiotokeza kwa wingi ni pamoja na takriri, balagha, tashbihi, taashira, chuku, na methali. Mbinu hizi zilichangia pakubwa katika kuziboresha nyimbo zilizotungwa na wasanii hawa na ambazo ziliteuliwa katika utafiti huu.

Sura ya nne imehakiki ulinganifu uliopo katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za Daudi Kabaka na kundi la Maroon Commandos. Katika sura hii, vipengele mbalimbali vya kifasihi viliweza kutumiwa katika kubainisha mahusiano yanayojitokeza katika

nyimbo za waimbaji hawa wawili. Baada ya kuhakiki nyimbo zao, ilibainika kuwa nyimbo hizo zilishabihiana pakubwa baada ya kuangalia vigezo kama mazingira, utamaduni, mwingiliano wa maudhui, uteuzi wa lugha, mtindo wa usimulizi na usawiri wa wahusika.

Sura ya tano imeshughulikia muhtasari wa utafiti, hitimisho na pia kutoa mapendekezo ya tafiti zingine za baadaye zenye uhusiano na utafiti huu.

**5.2 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulidhamiria kubainisha maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili: Mtazamo linganishi wa msanii Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia ya uhalisia ni nadharia inayotumiwa kulinganisha fasihi na kioo cha jamii. Dhima kuu ya mtunzi wa nyimbo ni kuisawiri jamii jinsi ilivyo. Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida wanaopatikana katika jamii halisi, kuchunguza na kusimulia maisha yao, tajiriba zao na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Kwa mujibu wa nadharia hii, jamii ya waswahili iliyolengwa na waimbaji Daudi Kabaka na wana Maroon imewasilishwa kikamilifu kama ilivyo hakikiwa kupitia tamaduni zao, mila, desturi, tabia na mienendo yao.

Kupitia uchanganuzi wa maudhui katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili, ni wazi kwamba masuala yanayozungumziwa katika nyimbo hizi yalikuwepo miaka ya elfu moja kenda mia na sitini wakati ambapo nyimbo hizi zilipoanza kutungwa na kuimbwa na yanaendelezwa na jamii ya karne ya ishirini na moja. Udaku au umbeya ambayo ni tabia ya kuchunguza habari za watu ni maudhui yaliyoungwa mkono na watu wengi

waliohojiwa. Baadhi yao waliongezea kuwa, (japo kwa mzaha) nyimbo za aina hii zinapaswa kuchezwa hata katika sehemu za maabadi kwani udaku umeshamiri sana hata makanisani. Hii ni tabia ambayo imechangia pakubwa kuvunjika kwa ndoa katika jamii ya karne ya ishirini na moja. Maudhui mengine yaliyofafanuliwa katika kazi hii ni pamoja na ukosefu wa kazi, kutelekezwa kwa watoto, ombaomba mitaani, uvivu, mafarakano katika ndoa na mapenzi. Maudhui haya yamechangia katika kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu kwani haya ni mambo yanayoshuhudiwa katika jamii halisi ikikumbukwa kwamba dhima kuu ya uhalisia ni kubainisha jamii jinsi ilivyo.

Kupitia tamathali za usemi na mchango wake katika uwasilishaji wa maudhui, ilibainika kuwa tamathali mbalimbali za lugha ziliweza kutumiwa na wasanii hawa ili kupigia mfano maisha halisi ya binadamu. Ilidhihirishwa kuwa nadharia ya uhalisia hulinganisha fasihi na maisha ya wanajamii. Tamathali za lugha zilizotumika katika nyimbo zilizoteuliwa katika utafiti huu ni kama vile takriri, balagha, tashbihi, taashira, chuku na methali. Tamathali hizi hutilia nguvu ujumbe unaopitishwa katika nyimbo hizi na kuyakuza maudhui yake kwa kuyawasilisha kwa njia yenye mvuto zaidi. Hivyo basi, lengo hili liliweza kufanikiwa na kuafikiwa kama ilivyobainishwa kwenye sura ya tatu.

Lengo la tatu la utafiti huu lilihusu ulinganifu unaojitokeza katika nyimbo zilizopendwa za Kiswahili za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos. Kupitia lengo hili, iligunduliwa kuwa vipengele mbalimbali vinaweza kutumiwa katika kuhakiki namna kazi za fasihi zinavyoweza kulingana ama kutofautiana. Nyimbo za wasanii hawa zimelingana katika mambo mengi mathalani mazingira ya mtunzi, utamaduni, mwingiliano wa maudhui, uteuzi wa lugha, mtindo wa usimulizi na usawiri wa wahusika. Ijapokuwa vipo

vipengele vingine vinavyoweza kutumiwa katika kuhakiki ulinganifu wa watunzi, vipengele hivi vilivyotumiwa katika sura ya nne vimechangia kwa asilimia kubwa katika kufanikisha lengo hili.

Hivyo basi, utafiti huu umefanikiwa katika malengo yake yote na nadharia iliyoteuliwa imechangia kufanikisha maudhui katika nyimbo zilizopendwa na Kiswahili za Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos kwa kuyaangazia maisha ya wanajamii jinsi yalivyo.

**5.3 Matatizo**

Utafiti wowote ule haukosi changamoto ambazo mtafiti hukumbana nazo. Katika kazi hii, uhaba wa hela ulimkumba mtafiti kwani maeneo ya kukusanya data hasa nyanjani yametengana sana. Miji ya Machakos, Nairobi na Mombasa i mbali kwa hivyo gharama za usafiri zilikuwa juu sana. Vilevile, maeneo mengi ya burudani uhudhuriwa sanasana nyakati za jioni ama usiku baada ya kazi na ili kukutana na watafitiwa lazima utembelee maeneo hayo nyakati hizo. Isitoshe, takribani sehemu zote za burudani huwa zimeandikwa *"No idle sitting"* yaani usikae hapa bila kuhudumiwa (tafsiri yetu). Hili linamaanisha kuwa lazima mtafiti awe na pesa za kutosha za kulipia huduma zinazotolewa katika maeneo hayo ya burudani.

Changamoto nyingine iliyokumba utafiti huu ni kuwa, idadi kubwa ya watu waohudhuria maeneo ya burudani ambako nyimbo zilizopendwa za Kiswahili huchezwa ni watu wazima walio na umri wa miaka zaidi ya thelathini na mitano. Ilibainika kuwa vijana wengi walio na chini ya miaka thelathini uhudhuria sehemu zinazocheza mitindo tofauti ya nyimbo hasa za Kiingereza na ambazo huchezwa kwa kutumia vifaa vya kisasa vya

kielektroniki tofauti na watu wazima ambako waimbaji hutumbuiza hadhira moja kwa moja kwa kuimba nyimbo hizo na pia kucheza vyombo vyenyewe. Hata hivyo, vijana waliohojiwa walifanikisha utafiti huu.

Tatizo lingine ambalo lilikumba utafiti huu ni kuwa, nyimbo nyingi zilizoteuliwa katika utafiti huu hazijahifadhiwa katika maandishi. Baadhi ya mistari ya nyimbo hizo imewekwa katika mtandao hasa "*YouTube*". Mtafiti alilazimika kusikiliza nyimbo ambazo hazijahifadhiwa kimaandishi na kunakili kwenye kijitabu jambo ambalo lilichukua muda mwingi sana.

**5.4 Mapendekezo**

Utafiti kuhusu nyimbo zilizopendwa za Kiswahili umefanyiwa utafiti ambao si mwingi sana. Katika utafiti huu, mtafiti alijifunga katika nyimbo za kikundi cha Maroon Commandos na Daudi Kabaka ili kuangazia maudhui katika nyimbo zao. Kuna baadhi ya masuala mengi ambayo utafiti huu haujashughulikia.

Kwanza, ikiwezekana litakuwa jambo la busara endapo mtafiti mwingine atafanya utafiti kuhusu mwingiliano matini katika nyimbo zingine zozote za kale na za sasa. Utafiti huu huenda ukathibitisha sababu za nyimbo zilizopendwa za Kiswahili kuanza kuimbwa upya na waimbaji wengine wa baadaye ambao huchukua maneno yaleyale ya nyimbo hizo na kuziimba kwa mtindo unaofanana na wa waimbaji asilia.

Pili, mtafiti anaweza kufanya utafiti ili aweze kubainisha sababu mbalimbali zinazofanya nyimbo zilizopendwa za Kiswahili ziwe na hadhira inayozidi kupanuka kila siku licha ya kuwa ziliimbwa kuanzia miaka ya elfu moja tisa mia na sitini. Kwa kufanya hivyo utafiti wa aina hii huenda ukatoa mwongozo kwa watunzi na waimbaji wa karne ya ishirini na

moja na vipindi vya baadaye kuhusu vipengele vya kuzingatiwa ili wimbo huenziwe na vizazi vya baadaye na kuweza kudumu kwa muda mrefu.

Utafiti huu aidha, ulitumia nadharia ya Uhalisia. Litakuwa jambo la busara endapo mtafiti mwingine atatumia nadharia tofauti kama vile nadharia ya mwingiliano matini au naratolojia kubainisha maudhui katika nyimbo zilizopendwa za wasanii wa kale kama vile Fundi Konde, Fadhili Williams, David Amunga, John Nzenze na waimbaji wa baadaye kama kikundi cha Them mushrooms ambacho kiliziimba tena upya nyimbo hizo.

## MAREJELEO

Akuno, E.(1999). A Conceptual Framework for Research in Music in Education Within a Cultural context.Paper presented at Cultural week seminar,Kenyatta University:Nairobi.

Bebey,F.(1975)..*African Electronic Music*.Younde:Cameroon press.

Bostock, D. (2000).*Aristotles Ethics.* New York: Oxford University Press.

Boyels,N.& Swales, M. (1986). *Realism in European Literature*. London: Cambridge University Press.

Brandel,R.(1959).*The Music of Central Africa*.An EthnomusicologicalStudy. London:Methuen

Chesaina,C.(1994).*Oral Literature of the Kalenjin.*Nairobi:East African Educational PubishersLimited.

Chiuri, J. (1984). Pop Music as a Form of Oral Literature: A Survey on John Kamaru. *Tasnifu ya PGDE:Chuo Kikuu cha Nairobi*.

Finnegan, M. (1977*). Oral Poetry.* Cambridge:Cambridge University Press.

Jacobson, J. W. (1960). “Concluding statement: Linguistics and Poetics”, Katika Seboek, J. (Mh), *Style and Language*. Cambridge: MIT.

Kabira, W. na Karega, M. (1988). *Gikuyu Oral Literature.* Nairobi: Heinemann Kenya Limited.

Keenan, F. (1996). *Virtues of Ordinary Christians*. Sheed and Ward Publishers.

Keesey, D. (1987).*Contexts for Criticism*. New York: Mayfield pub Co.

King'ei, G. na Kisovi,M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi***.** Nairobi: Kenya Literature Bureau.

King'ei, G. (1992).Language, Culture and Communication**.** The Role of Swahili Taarab Songs in Kenya from 1963-1990. *Unpublished PhD. Dissertion: Horward University.*

Kipuri, N. (1983).*Oral Literature of the Maasai*.Nairobi:Heinemann Educational Books.

Maitaria, J. (2012). Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali. *Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa)*:*Chuo Kikuu cha Kenyatta*

Malenya, M. (2008). Matumizi ya Lugha na Jazanda Katika Nyimbo za Jacob Luseno.*Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Kenyatta*.

Mazrui, A. na Syambo,K. (1992).*Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbatia, M. (2001).*Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Fotoform Limited.

Msokile, M. (1992).*Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.

Mue, E. (2013).Maudhui na Matumizi ya Lugha Katika Nyimbo za Injili za Rose Mohando. *Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Kenyatta*.

Mwamanda, J. (2008).*Nadharia yaFasihi, Uchambuzi na Uhakiki*. Dar es Salaam: JPD Company & General Supplies limited.

Ngugi,P.(2000). Nafasi ya Muziki Uliopendwa katika Fasihi ya Kiswahili. Swahili Forum VIII(145-152).

Ngure, A. (2003*). Fasihi Simulizi*.Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Ntaragwi, M. (1990). Maudhui Katika Nyimbo za Remi Ongara. *Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa):Chuo Kikuu cha Kenyatta.*

Odidi, B. (2014, December 1). In what Direction is Kenyan Music Heading? *Daily Nation*.

P'Bitek,O. (1973).*African's Cultural Revolution*. Nairobi: Macmillan.

Senkoro, F. (1982).*Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Wafula,R. na Njogu, K.(2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.*Nairobi:Jomo Kenyatta Foundation

Wamitila, K. (2002).*Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Wellek, R. (1961). The concept of realism in literary scholarship *Neophilologus, 45*(1), 1.

Wambua, S. (2001). Mtindo na Matumizi ya Lugha Katika Nyimbo za Kakai Kilonzo. *Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa):Chuo Kikuu cha Kenyatta.*

# VIAMBATISHO

## Kiambatanisho I: Nyimbo

**DAUDI KABAKA**

**SHAURI MOYO TWIST**

Nilikuta bibi wa kwanza Nairobi

Akanipenda na mimi nikampenda

Nikamwuliza kama ana bwana

Akanijibu sina hata mpenzi

Nilikuta bibi wa kwanza Nairobi

Akanipenda na mimi nikampenda

Nikamwuliza kama ana bwana

Akanijibu sina hata mpenzi

Tukaenda naye mpaka kwake

Shauri Moyo kwa nyumba za tumbako.

Nilipolala kasikia hodihodi,

Fungueni ni mimi mwenye nyumba

Tukaenda naye mpaka kwake

Shauri Moyo kwa nyumba za tumbako.

Nilipolala kasikia hodihodi,

Fungueni ni mimi mwenye nyumba

Bibi akileta aibu sanasana

Kuwaka mimi na yule bwana

Tungepigana mimi na yule bwana

Tuumizane weye ungefanyaje

Nilikuta bibi wa kwanza Nairobi

Akanipenda na mimi nikampenda

Nikamwuliza kama ana bwana

Akanijibu sina hata mpenzi

**POLE MUSA**

Musa nimevumilia sana

Musa nimevumilia sana

Kupigwa pigwa kama mimi punda

Na sura yangu imeharibika

Na ngumi zako za kila siku Musa

Taabu…taabu…tabu

Kweli Musa,uliponioa

Sura yangu haikuwa na alama hata moja

Nilikuwa na afya nzuri

Nilinona kama ngoima ya kirike

Kweli Musa,uliponioa

Sura yangu haikuwa na alama hata moja

Nilikuwa na afya nzuri

Nilinona kama ngoima ya kirike

Oyee oyee tafadhali Musa

Tafuta bibi atakayeweza

Kuvumilia hizo tabia zako

Ukinywa pombe wamunywea yeye

Ukinywa munyeke wamunywia yeye

Poleee… poleee…pole

**TAABU NI KWA MWANAMUME**

Ukizaliwa wewe ni kijana

Ukose kazi taabu yote itakupata

Ukizaliwa wewe ni kijana

Ukose kazi taabu yote itakupata

ooh darling Marina baby

Umeniacha ati sina kazi

ooh darling Marina baby

Umeniacha ati sina kazi

Ukizaliwa wewe ni kijana

Ukose kazi taabu yote itakupata

Ukizaliwa wewe ni kijana

Ukose kazi taabu yote itakupata

Ukienda kuona mtu wa kwenu

Ukitoka wanaanza masengenyo

Ukienda kuona mtu wa kwenu

Ukitoka wanaanza masengenyo

Huyu kijana kazi gani anataka,

Kupeleka ndege ama kupeleka gari

Huyu kijana kazi gani anataka,

Kupeleka ndege ama kupeleka gari

Ooh kazi ni ngumu mama

Nimetafuta sasa nimeshindwa.

Ooh kazi ni ngumu mama

Nimetafuta sasa nimeshindwa.

Lakini bwana wewe ukumbuke

Kazi ya mzungu lazima hutafutwa.

Lakini bwana wewe ukumbuke

Kazi ya mzungu lazima hutafutwa.

Ooh kazi ni ngumu mama

Nimetafuta sasa nimeshindwa.

Ukizaliwa wewe ni kijana

Ukose kazi taabu yote itakupata

Ukizaliwa wewe ni kijana

Ukose kazi taabu yote itakupata

**MSICHANA WA ELIMU**

Msichana wa sura nzuri

Kitu gani kinakufanya usiolewe?

Elimu unayo ya kutosha,

Hata ng’ambo ukaenda ukarudi

Msichana wa urembo kama wewe,

Huonyeshe mapenzi kwa vijana,

Ukionyesha majivuno kwa vijana,

Utazeeka ukiwa nyumbani kwenu

Oooh baby,

Miaka yaenda mbio sana,

Na sura yako ikizidi chujuka.

Oooh baby,

Miaka yaenda mbio sana,

Na sura yako ikizidi chujuka.

Pengine tabia zako ndizo mbaya,

Awali kweli dada ulijivuna,

Kwanza mimi nilitaka nikuoe,

Ukaringa hati sina masomo.

Oooh baby

Ona watoto wa nyuma yako,

Wameolewa wamekuacha ukiangaika

Oooh baby

Ona watoto wa nyuma yako,

Wameolewa wamekuacha ukiangaika

Msichana wa sura nzuri

Kitu gani kinakufanya usiolewe?

Elimu unayo ya kutosha,

Hata ng’ambo ukaenda ukarudi

**KABAKA SAYS-VIWETE**

Kuuliza jamani,si ujinga aah

Bali ni kujua mengi ya ulimwengu.

Hawa viwete wetu,wasiojiweza

Hebu niambieni hupata mtu na kamtoto

Mkikutana njianisauti ya mtoto,

Yenye huruma saidia maskini.

Mkikutana njiani sauti ya mtoto,

Yenye huruma saidia maskini.

Tutasaidia nani? Tusaidie nani? Tutasaidia nani?

mama na mtoto,aeeh mama na mtoto

Tukizaa na kipofu,mtu kizaa na kiwete,

Mtu kizaa na bubu chukua mtoto.

Aeeh mtoto si mjinga,aeeh mtoto si kipofu

Aeeh mtoto si kiwete,aeeh mtoto sio bubu.

Nasikitika kuuliza,wasiojiweza

Hawa hutungwa mimba na nani nijuwe,

Tusaidie maskini, mtoto na mama

Lakini huyu mtoto amezaliwa na nani?

Asiyejiweza ndiye baba wa mtoto

Au ni wa mtu mwenye akili zake.

Asiyejiweza ndiye baba wa mtoto

Au ni wa mtu mwenye akili zake.

Wanaume maskini huomba njiani,

Saidia maskini akishalewa pombe.

Mtu mwenye shida

Akipata kidogo, hutumia kwa shida zake

sio kulewa pombe

Tembea kila taoni wakati wa usiku

Maskini wanalala varandani za maduka.

Tembea kila taoni wakati wa usiku

Maskini wanalala varandani za maduka.

**SAFARI TANGANYIKA**

Masita, ninaenda safari Tanganyika

Usilie,machozi sana mimi nitakonda

Masita, nitarudi mpaka tuonane

Zippora baby Zippora shina Zippora { Shina- ni nini?}

Zippora baby Zippora shina Zippora

Usidhani, nitamwoa mwingine Tanganyika

Hata mimi, nikitembea nakuwaza Masita

Nifanyeje, safari yangu sa itavunjika

Nikorendi baby ni shida sheri kwa safari

Nikorendi baby ni shida sheri kwa safari { Nifanye nini baby ni shida ziko kwa safari}

Tanganyika, nilipata chotara akanipenda

Nikaona, rangi yangu nyeusi kumshinda

Kakumbuka, Masita wangu yuko Nairobi

Zippora baby Zippora shina Zippora.

**VIJANA WA MJINI**

Nalia nalia kilio na machozi

Nalia nalia kilio na machozi

Machozi yanitoka kwa vijana wa mjini

Mbona heshima ya taoni ni ndogo sana

Hamna hata shemeji mnajua Mueni ni wangu

Hamna hata shemeji mnajua Mueni ni wangu

Hiyoooo

Vijana wa mjini lilonge

Hamna hata shemeji jamani

Vijana wa mjini lilonge

Hamna hata shemeji jamani

Msiingilie Mueni wangu jamani

Mapenzi ni siri ya wawili

Msiingilie Mueni wangu jamani

Mapenzi ni siri ya wawili

Ningekwambia ninavyompenda Mueni

Ningekwambia ninavyompenda Mueni

George uache kutonesha moyo wangu

George uache kutonesha moyo wangu

Ukigusa Mueni wangu umegusa moyo wangu

Nyasaye mbohola minyololo gwa mwoyo gwange

makava sinyenyanga makono mavi sinyenyanga

Makava singenyanga makono mavi sinyenyanga

Vijana wa mjini lilonge

Hamna hata shemeji jamani

Msiingilie Mueni wangu jamani

Mapenzi ni siri ya wawili

**DAWA NIMUONE HANI**

Wenzangu nifanye nini, kwani mawazo yamenizidi

Wenzangu nifanye nini, kwani mawazo yamenizidi

Maanake mpaka leo, kuteseka juu ya hani

Maanake mpaka leo, kuteseka juu ya hani

Tulijaliwa watoto, tulipokuwa nayo mapenzi

Tulijaliwa watoto, tulipokuwa nayo mapenzi

Mpaka leo sijui, hani alipo

Mpaka leo sijui, hani alipo

Jamani nauliza, huyu hani kama yuko hai

Jamani nauliza, huyu hani kama yuko hai

Kumbe dawa nimuone hani, ndipo ziniache ndoto

Kumbe dawa nimuone hani, ndipo ziniache ndoto

Mpaka leo sijui, hani alipo

Mpaka leo sijui, hani alipo

Wezangu nifanye nini, kwani mawazo yamenizidi

Wezangu nifanye nini, kwani mawazo yamenizidi

Maanake mpaka leo,kuteseka juu ya hani

Maanake mpaka leo, kuteseka juu ya hani

Tulijaliwa watoto, tulipokuwa nayo mapenzi

Tulijaliwa watoto, tilipokuwa nayo mapenzi

Mpaka leo sijui, hani alipo

Mpaka leo sijui, hani alipo.

Kumbe dawa nimuone hani, ndipo ziniache ndoto

Kumbe dawa nimuone hani, ndipo ziniache ndoto

Kwani siku nyingi sana aa, sijamuona hani

Kwani siku nyingi sana aa, sijamuona hani

Wazee waliniambia, dunia ni mviringo

Wazee waliniambia, dunia ni mviringo

Milima haikutani, binadamu hukutana

Milima haikutani, binadamu hututana

Usife moyo kijana, kuna siku mtakutana

Usife moyo kijana, kuna siku mtakutana

**USINIAMBIE UNAENDA (MAROON COMMANDOS)**

Sitaki uniambie kuwa unaenda,

Haraka unajua haina baraka,

Subiri kidogo nikueleze,

Usiniache nibaki na wasiwasi,

Mpenzi sikia mambo yangu…

Naumia sana juu yako mama..

Sitaki…sitaki….sitaki….sitaki

Tukipatana wewe husema una haraka..

Ya nini unitese bila sababu..uu,

Fikiria kwa makini ninayosema mama,

Usiniweke kwa hali hii mpenzi wee,

Aye mama wee..

Sitaki uniambie kuwa unaenda,

Sitaki unambie kuwa unaenda,

Kwani nimeshakuzoea nibaki na nani?

Sitaki unambie eti unaenda.

**EWE SOFIA**

Mimi nakujulisha

Ukae ukijua

Kwamba hapa nilipo

Nilimwoa mwingine hivi majuzi

Ewe sofia

Ukae ukijua

Kwamba hapa nilipo

Nilimwoa mwingine hivi majuzi.

Mimi sina shaka mama watoto

Mimi sina shaka mama watoto

Watoto uliowaacha wako salama

Watoto uliowaacha wako salama

Yote uliyoyataka hayakuwa

Yote uliyoyataka hayakuwa

Hawa watoto wangu sitatupa

Hawa watoto wangu sitatupa

Hata ufanye nini hautawapata

Hata ufanye nini hautawapata

**RIZIKI**

Eeh mwana aa, sikiliza nikweleze,

Usijisukumie mambo makubwa,

Mapato yako ni madogo,yafaaa uyapange

Haba na haba,hujaza kibaba

Huyo mwenzio ashabahatika…

Hiyo riziki yake  ishamfikia

Kazana kazana mwana

Na mwisho utafanikiwa

Usiibe wala usinyang'anye

Vya kuiba havina baraka.

Kazana…kazana mwana

Pengine utafanikiwa

Riziki riziki mwana

Haivutwi na kamba.

**SOFIA**

Sofia eeh Sofia,mwana mama,

Sofia umetenda mambo mabaya,

Sofia umewacha eeh,watoto wako,

Sawa na kuwatupa eeh,watoto wako

Watoto uliwazaa,kwa nini uwawache?

Rudi nyumbani Sofia eeh,aeeh,

Rudi kaone watoto ooh,

Rudi nyumbani Sofia aeeh,

Rudi kaone watoto ooh

Rudi nyumbani Sofia eeh…aeeh,

Rudi kaone watoto…

Punguza zako hasira aeeh,

Rudi kaone watoto…

Watu hukosana kila mara…

Wakasameheana eeh…

Rudi nyumbani Sofia,

Rudi kaone watoto wako.

**UVIVU**

Uvivu ni adui mkubwa, wa ujenzi wa taifa

kwani ndicho kiini hasa, kisababishacho njaa.

Ewe ndugu yangu wee, amka kumekucha

kamata jembe na panga,twende shamba.

Hata wewe mwanangu, amka kumekucha

kwani hizi ndizo saa, za kwenda shule.

Hata wewe karani, amka kumekucha

kwani hizi ndizo saa, za kwenda kazi.

Uvivu ni adui mkubwa, wa ujenzi wa taifa

kwani ndicho kiini hasa, kisababishacho njaa

Ewe ndugu yangu wee, amka kumekucha

kamata jembe na panga, twende shamba

Hata wewe mwanangu, amka kumekucha

kwani hizi ndizo saa, za kwenda shule

Hata wewe Karani, amka kumekucha

kwani hizi ndizo saa, za kwenda kazi

Uvivu ni adui mkubwa, wa ujenzi wa taifa

kwani nicho kiini hasa, kisababishacho njaa

Ewe ndugu yangu wee, amka kumekucha

kamata jembe na panga,twende shamba

Hata wewe mwanangu, amka kumekucha

kwani hizi ndizo saa, za kwenda shule

hata wewe karani, amka kumekucha

kwani hizi ndizo saa, za kwenda kazi

Uvivu ndio adui, wa ujenzi wa taifa

jiepushe na uvivu, tujenge taifa

Ndugu yangu kumekucha, amka twende shamba

jiepushe na uvivu, tujenge taifa

mwanangu kumekucha, amka uende shule

Elimu ndio msingi, wa maendeleo

Karani kumekucha, amka uende kazi

jiepushe na uvivu, tujenge taifa

uvivu ndio adui, wa ujenzi wa taifa

jiepushe na uvivu, tujenge taifa

ndugu yangu kumekucha, amka twende shamba

jiepushe na uvivu, tujenge taifa

mwanamke kumekucha, amka uende shule

elimu ndio msingi, wa maendeleo

Karani kumekucha, amka uende kazi

jiepushe na uvivu, tujenge taifa

hata wewe arani, amka kumekucha

kwani hizi ndizo saa, za kwenda kazi

**DADA MDAKU**

Mwenendo wako sio mwema, ewe dada jirekebishe,

Mwenendo wao sio mwema, ewe dada jirekebishe,

Ya nini kuzururazurura, umefahamika

Ya nini kuzururazurura, umefahamika

Umevuruga nyumba nyingi, na kwetu usije tena

Tafuta kijana wa hapo kwenu, awe rafiki yako utulie.

Tafuta kijana wa hapo kwenu, awe rafiki utulie.

Wana maroon wameshaona mambo yako si mazuri

Tabia zako wewe sio nzuri,bora tukueleze waziwazi

Wewe dada umdaku tena sana, waingia nyumba hii hadi nyingine.

Wana maroon wameshaona mambo yako si mazuri

Tabia zako wewe sio nzuri, bora tukueleze waziwazi.

Wewe wawasha moto kila nyumba, kisha wajifanya u mzuri,

Wana maroon wameshaona mambo yako si mazuri

Tabia zako wewe sio nzuri, bora tukueleze waziwazi.

**KRISTINA**

Kristina dada

Uko wapi?

Nakutafuta sikuoni

Nimejaribu sana kukutafuta

Na kila nifikapo sikuoni

Lakini kwa bahati umenikumbuka

Kwani barua uliyoituma nimeipata

Sasa nakuomba unieleze

Siku ambayo utafika.

Sasa nakuomba unieleze

Siku ambayo utafika

Siku gani dada

Utakuja

Nikungojee

Sitesheni

Ningekuwa na uwezo

Ningekutumia nauli ya ndege

Ili ufike haraka

Nimekukosa mama

Nimekukosa siku nyingi

Siku gani dada

Utakuja

Nikungojee

Sitesheni

Ningekuwa na uwezo

Ningekutumia nauli ya ndege

Ili ufike haraka

Nimekukosa mama

Nimekukosa siku nyingi

**Kiambatanisho II: Hojaji**

Jina………………………………………….. Jinsia…………

Eneo……………………………………..

Umri……………………………………..

Maswali yafuatayo yanalenga kumsaidia mtafiti kukusanya data kuhusu nyimbo zilizopendwa za Kiswahili.Nyimbo zinazorejelewa hapa ni za Daudi Kabaka na Maroon Commandos.

(a) Wafahamu wasanii Daudi Kabaka na kikundi cha Maroon Commandos?

………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(b) Ikiwa ndio, taja baadhi ya nyimbo zao maarufu.

………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(c) Kwa maoni yako, kwa nini nyimbo hizi ni maarufu?

………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

(d) Je, nyimbo hizi zina umuhimu wowote kwa jamii ya sasa?

………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………